**Shahidi** aangua kilio kizimbani kesi ya Sabaya

UKURASA 3



**Wafungua** shauri kupinga tozo za miamala ya simu

UKURASA 5




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Agosti 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580665

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Walia uhaba wa majeneza

**BAADHI** waahirisha maziko ya ndugu, watengenezaji wafanya kazi usiku na mchana... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akipanda kwenye basi la Jeshi la Magereza kurudi mahabusu Ukonga, baada ya kesi inayomkabili ya ugaidi kuahirishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



UKURASA WA 2

## WAFANYA UDANGANYIFU WAPATE CHANJO YA CORONA

KUMEIBUKA kundi la vijana wenye umri chini ya miaka 50 jijini Mwanza walioamua kuchangamkia huduma ya kupata chanjo ya UVIKO 19 wakidaiwa kusingizia wanaumwa magonjwa sugu ili kupewa kipaumbele....

UKURASA WA 4

## WHO YATAJA SABABU ZA ONGEZEKO VIFO CORONA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema vifo vya corona vimekuwa vingi awamu hii kwa sababu watu wamekuwa wakifika hospitalini wakiwa wanaumwa kwa kiwango kikubwa huku mapafu yakiwa yameshaharibika. Mtaalamu anayeshughulikia matatizo ya corona na kujikinga dhidi ya janga hilo, Dk. Nemes Iriya, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati shirika hilo likizungumza...

# Mawakili tisa kumtetea Mbowe, kesi kupelekwa Mahakama Kuu

UKURASA 2

# Rais Samia alivyoongoza mazishi ya Kwandikwa

UKURASA 3




Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza viongozi mbalimbali na wananchi kuaga mwili wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, marehemu Elias Kwandikwa, katika Viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **SIMBA MAWINDONI CAF** UK. 24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Wadanganya kupata chanjo

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KUMEIBUKA kundi la vijana wenye umri chini ya miaka 50 jijini Mwanza walioamua kuchangamkia huduma ya kupata chanjo ya UVIKO 19 wakidaiwa kusingizia wanaumwa magonjwa sugu ili kupewa kipaumbele.

Makundi yanayopewa kipaumbele katika kupata chanjo ya UVIKO 19 kwa sasa ni pamoja na watu wenye umri zaidi ya miaka 50, wenye magonjwa sugu na watumishi wa sekta ya afya.

Vijana hao wamelazimika kudanganya umri ama kusingizia kwamba na wao wana magonjwa sugu ili wapate chanjo ya corona ambayo ilianza kutolewa mapema wiki hii mkoani Mwanza.

Akizungumza na Nipashe jana katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure), Muuguzi Mfawidhi wa hospitali hiyo, Uyanjo Nkumbi, alisema kundi hilo linatumia mbinu hizo ili kupata chanjo.

Hata hivyo, alisema tayari wameshabaini tatizo hilo, lakini vijana hao wanapobainika kwenye kituo kimoja, huhamia kwenye kituo kingine kufanikisha lengo lao.

"Wale wenye magonjwa sugu kama kisukari, presha, UKIMWI na kansa ndiyo wanaopewa kipaumbele katika kuchanjwa, lakini kutokana na baadhi ya watu kudanganya, takwimu zitaonyesha idadi kubwa ya vijana wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 50 wana magonjwa sugu," alisema. Alisema idadi ya wagonjwa ambao wanahudumiwa kwa siku moja katika kituo hicho ni zaidi ya 200 na kwamba kuanzia Jumatatu wiki hii hadi jana, walikuwa wamehudumia watu zaidi ya 700.

Alibainisha kuwa chanjo zilizopelekwa kwenye kituo chao ni 3,050 na kwamba katika Wilaya ya Nyamagana vipo vituo vitano ambavyo vinatoa huduma hiyo.

Kaimu Mganga Mfawidhi katika Hospitali hiyo, Dk. Athanas Ngambakubi, alisema kuna baadhi ya watu ambao walijitokeza siku ya kwanza na hawakupata chanjo kwa kuwa hawakukidhi vigezo.

"Kumtambua mtu mwenye ugonjwa sugu haihitaji mtu kupimwa, busara pia inaweza kutumika kwa wale wanaoonyesha uhitaji wa chanjo wanapewa ushauri, siku ya kwanza wapo waliorudishwa kutokana na kutokukidhi vigezo," alisema.

# Majeneza yaadimika

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HUDUMA za mazishi na uuzaji wa majeneza kwenye Mji wa Moshi zimetajwa kuongezeka katika siku za karibuni.

Kutokana na ongezeko hilo, baadhi ya watoa huduma wameiomba serikali kuona namna ya kuwasaidia wasilipe kodi na tozo mbalimbali kwa kuzingatia wanatoa huduma na sio biashara.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti mjini hapa, baadhi ya watoa huduma hao, akiwamo France Temba wa Mtaa wa KCMC, walisema kwa sasa majeneza yamekuwa yakitoka kwa wingi kiasi cha kuwalazimu kufanya kazi mchana na usiku.

"Kwa hapa kwetu majeneza yanaanzia Sh. 150,000 hadi 1,000,000. Kwa sasa yanachukuliwa sana, yaani kwa siku yanatoka matano mpaka tisa hasa ya kuanzia Sh. 400,000 kurudi chini wakati huko nyuma yalikuwa yakitoka mawili hadi matatu kwa wiki.

"Hii ina maana kwamba watu wanakwenda (wanafariki dunia) na ni wale wa hali za maisha ya kawaida," alibainisha.

Mtoa huduma huyo alisema upatikanaji wa malighafi, ikiwamo mbao, rangi na urembo, umekuwa mgumu, hivyo wanaomba serikali ifikirie kuwapunguzia gharama.

Elinasari Nkyini alisema: "Sisi hutengeneza majeneza usiku na mchana, tumeongeza vijana wa kazi, kuna siku watu wanakuja wanane hadi 14 wakitaka majeneza ya kesho yake au siku mbili mbeleni, hivyo inatulazimu kuhakikisha huduma inapatikana lakini tunakabiliwa na matatizo mengi kwa sasa ikiwamo upatikanaji wa malighafi."

Mkurugenzi mwenza wa kampuni ya huduma za mazishi ya Godmark, Lucas Gondwe, alisema kwa takribani miezi miwili sasa, biashara imebadilika ghafla na uhitaji umekuwa mkubwa tofauti na kipindi cha nyuma.

Alisema kwa sasa wanatoa majeneza matatu hadi manne kwa siku, ambapo awali walikuwa wanatoa idadi hiyo kwa wiki.

"Katika kampuni yetu tunatoa huduma hiyo kwa gharama za kuanzia Sh. 400,000 hadi 4,000,000, inategemea na ubora na malighafi zilizotumika.

"Kwa sasa ipo haja serikali kuona namna ya kuwasaidia watoa huduma za mazishi nchini ili watoe huduma bora kwa kwa wahitaji.

"Kwa sasa tunachajiwa kodi kubwa, malighafi zimekuwa ghali, ulipaji wa pango, leseni za biashara, watu huja hapa bila pesa na tunalazimika kuwapa huduma baada ya mazishi walete hela, cha ajabu wengine hata simu hawapokei tena," alisema.

Baadhi ya wananchi walioukuwa wakipatiwa huduma ya majeneza katika barabara ya KCMC, akiwamo Faustina Kimario, walisema kwa sasa huduma ya majeneza imekuwa ngumu kuipata.

"Sisi tuliweka oda ya jeneza la kumzika ndugu yetu juzi lakini tumefika hapa leo (jana) bado halijaandaliwa na tumelazimika kuahirisha shughuli yetu hadi Jumamosi, tumezunguka kutafuta hakuna yaliyopo tayari, serikali iangalie suala hili.

"Kwa sasa ukipatwa na msiba, kabla ya kwenda kutafuta viongozi wa dini au kukaa kikao cha familia, inabini uende kwanza kutafuta jeneza, inasikitisha inahuzunisha, tunapoelekea watu wanaweza kuzikwa bila majeneza," alisema Zawad Mlay.

# Mawakili kesi ya Mbowe wafika 9

**Na Kulwa Mzee**

MAWAKILI wanaomtetea Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake wamefika tisa, Jamhuri ikiwasomea mashtaka upya huku Mahakama ikiamuru waletwe baada ya siku saba kwa ajili ya kusomewa maelezo ya ushahidi.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, ilifikia uamuzi huo jana baada ya Jamhuri kuwasomea washtakiwa mashtaka sita ya ugaidi na kudai upelelezi umekamilika na jalada la kesi liko kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, hivyo tarehe itakayopangwa, watawasomea washtakiwa maelezo ya mashahidi.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, Christopher Msigwa, na Sylvia Mintato.

Upande wa Utetezi uliwakilishwa na Mawakili Peter Kibatala, Lwekamwa Rweikiza, John Mallya, Fredrick Kihwelo, Selemani Makoweka, Michael Rugina, Iddi Msawanga, Jebra Kambole na Sisty Aloyce.

Jeshi la Polisi liliimarisha ulinzi, askari wakizingira mahakama, ndani na nje ya lango kuu na katika barabara zote zilizoizunguka mahakama hiyo huku magari yenye maji ya kuwasha yakiwa yameegeshwa nje ya uzio.

Ulinzi huo ulifanya idadi ya wafuasi wa CHADEMA kupungua kulinganisha na ya waliofika kwenye mahakama hiyo juzi.

Wakili Hillar aliifahamisha Mahakama kwamba kesi ilikuja kwa ajili ya kutajwa, washtakiwa wote walikuwapo na upande wao walikuwa tayari kuwasomea washtakiwa hao hati mpya ya mashtaka.

Alidai Julai 26, mwaka huu, Mbowe alisomewa mashtaka akiwa peke yake na Julai 27 washtakiwa wengine watatu waliokuwa katika kesi hiyo waliachiwa na kufanya idadi ya washtakiwa kubakia wanne badala ya saba.

Wakili Hillar aliwasomea mashtaka sita ya ugaidi tofauti na hati ya mashtaka ya awali iliyofunguliwa Agosti, mwaka 2020 iliyokuwa na mashtaka 13, katika hati mpya mashtaka mawili ya kukutwa na dawa za kulevya aina ya Heroine yaliondolewa na mashtaka mengine matano ya kughushi nyaraka za benki yaliondolewa.

Akisoma mashtaka, Hillary aliwataja washtakiwa kuwa ni Mbowe, Halfan Hassan, Adam Kasekwa, maarufu Adamo na Mohamed Lingwenya, ambao wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 63/2020.

Alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita, katika shtaka la kwanza wanadaiwa wote, walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katika Hoteli ya Aishi iliyoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali huko, aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Lingwenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamuhuri ya Mauungano wa Tanzania.

Katika shtaka la tatu, washtakiwa Halfani, Adamu na Lingwenya wanadaiwa kukusanya fedha kutoka kwa Mbowe wakiamini zitasaidia kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko.

Katika shtaka la nne, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5 mwaka 2020, eneo la Rau, alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger bila kuwa na kibali.

Mshtakiwa Adamu anadaiwa katika shtaka la tano kuwa siku na mahali huko,alikutwa na vilipuzi ambavyo ni risasi tatu bila ya kuwa na leseni.

Mshtakiwa Halfani anadaiwa Agosti 10, mwaka 2020, kwamba kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi, alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kinyume cha sheria.

Vifaa hivyo anavyodaiwa kuvitumia ni suruali moja ya JKT pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana moja, koti la mvua moja, jaketi moja, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

Baada ya kumaliza kusoma mashtaka hayo, Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi umekamilika, jalada la kesi liko kwa DPP kwa ajili ya kuwasilisha taarifa mahakamani, washtakiwa wasomewe maelezo ya ushahidi kisha kesi ihamie Mahakama Kuu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Akijibu hoja hizo, Wakili Kibatala alidai upande wao unaomba Jamhuri wasome maelezo ya mashahidi haraka ili washtakiwa wajue hatima yao na aliomba kesi ipangwe tarehe ya karibu.

Kibatala alidai viongozi wa umma, akiwamo kiongozi wa wapelelezi nchini, walisikika wakisema washtakiwa wamefanya matendo ya ovyo ovyo, akidai kuwa hiyo ina maanisha kila kitu kuhusu upelelezi kiko tayari.

Hakimu Simba alisema kesi iko mahakamani tangu Agosti, mwaka jana, washtakiwa wengine walikuwa ndani kwa kipindi chote hicho na kwa kuwa upelelezi umekamilika, kila kitu kifanywe kwa haraka.

"Ipangwe tarehe ya karibu, kesi hii ina mvuto kwa jamii, hilo liko wazi, watu wengi wanasimama kufanya shughuli zao kwa ajili ya hii kesi," alisema Hakimu Simba na kuamuru washtakiwa waletwe mahakamani Agosti 13, kwa ajili ya Jamhuri kuwasomea maelezo ya mashahidi katika kesi hiyo.

Baada ya kusomwa kwa maelezo hayo, kesi hiyo itahamishiwa Mahakama Kuu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

HABARI KITAIFA

# Rais Samia alivyoongoza mazishi ya Kwandikwa

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan jana aliwaongoza viongozi mbalimbali na waombolezaji kuaga mwili wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, aliyefariki dunia mwanzoni mwa wiki.

Akizungumza wakati akitoa salamu za pole kwenye mazishi hayo Dar es Salaam jana, Rais Samia alisema kifo cha Waziri Kwandikwa kimeacha simanzi na pengo kubwa si kwa familia pekee, bali pia kwa serikali na taifa kwa ujumla.

Rais Samia alisema serikali imempoteza mtumishi na kiongozi mwadilifu, makini, shupavu na mchapakazi hodari, akibainisha namna alivyoshtushwa na taarifa za kifo cha kiongozi huyo alizozipokea akiwa ziarani Rwanda.

Mkuu wa Nchi aliwashukuru viongozi wa dini kwa kuongoza ibada ya kuuaga mwili wa Waziri Kwandikwa kwa mahubiri yao yaliyotoa faraja na kukumbusha kuwa wanadamu duniani wanapita, hivyo kutakiwa kuishi kwa wema na kutenda yale ya kumpendeza Mungu.

Shughuli za kuaga mwili wa Marehemu Kwandikwa zilifanyika kwenye Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali akiwamo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, Katibu Mkuu Kiongozi-Zanzibar, Zena Said, pamoja na viongozi wengine wa vyama vya siasa na serikali.

# Shahidi aangua kilio kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa nane wa Jamhuri, Magdalena Malya au Zulpha (32), katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ameangua kilio kizimbani akidai Sabaya alimnyooshea bastola akitishia kumuua yeye na mume wake, Bakari Msangi.

Mbali na Sabaya (34), washtakiwa wengine wawili katika kesi hiyo ya madai ya unyang'anyi wa kutumia silaha ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura(38).

Shahidi huyo ambaye ni mke wa Bakari Msangi, shahidi wa sita katika kesi hiyo, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, alidai kuwa Februari 9, mwaka huu, alipata udhuru ya kutokwenda kazini kwa kuwa alikuwa mgonjwa pamoja na mtoto wa kiume mwenye umri wa miezi saba.

Shahidi huyo, ambaye ni mwalimu, alidai kuwa akiwa mgonjwa na yuko nyumbani, mume wake alikuwa kwenye majukumu ya kila siku.

Majira ya saa nane akiwa nyumbani, alidai kuwa mume wake alimpigia simu kumjulisha kwamba kwenye mtaa wao kuna msiba, hivyo atakwenda kuzika lakini alimuuliza kuwa kama angefika nyumbani na mume wake alimweleza kwamba hawezi kupitia nyumbani kwa kuwa akimaliza kuzika atarejea kazini kwake.

Alidai majira ya saa 10 jioni, Februari 9, mwaka huu, alimpigia simu mume wake kumweleza kuwa dawa iliyokuwa ikitumiwa na mtoto wao imekwisha, hivyo wakati akirejea nyumbani kutoka kazini apitie duka la dawa kununua dawa nyingine.

"Majira ya saa moja kasoro mtoto alizidiwa kwa kuwa muwe wangu aliniambia anaingia msikitini kuswali, ilipofika majira ya saa 1:30 hadi saa 2:30 usiku nilimpigia simu aharakishe kuleta dawa hiyo, lakini nilipiga simu mara nyingi na haikupokewa.

"Ilipofika saa 3:00 usiku niliendelea kumpigia simu kwa wakati huo simu yake haikupatikana kabisa hivyo nikaanza kupata hofu. Niliendelea kujaribu kupiga simu na ilipofika majira ya saa 4:30 usiku mimi na watoto wangu tuliendelea kumsubiri bila mafanikio.

"Ilinibidi kuwalazimisha watoto kwenda kulala kwa nguvu kwa kuwa walikuwa wakimsubiri baba yao. Niliendelea kuwa na hofu kwa kuwa si kawaida yake kuchelewa nyumbani pasipo kutoa taarifa.

"Ilipofika majira ya saa 5:00 alinipigia simu mwenyewe na nilimuuliza yuko wapi na wakati huo alikuwa akizungumza kwa sauti ya chini kama amejificha sehemu. Aliniambia tangu majira ya saa 11:00 jioni amekamatwa na kushikiliwa na Sabaya na amempiga sana na hali yake ni mbaya. Nilimuuliza ni Sabaya yupi aliyekufanyia kitendo hicho, alinijibu kuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Hai," alidai.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa mume wake alimweleza amtafute jirani mmoja ambaye atamsindikia Tulia Lodge iliyoko Sakina kwa kuwa asingeweza kwenda mwenyewe kwa kuwa alikuwa mgonjwa .

"Aliniambia nifanye haraka nifike Tulia Lodge na nikifika hapo nimuulizie kwa kuwa Sabaya hakufahamu kama aliwasiliana na mimi na jirani yangu. Tulipofika hapo, kulikuwa na magari mengi yakiwa yamepakiwa eneo hilo. Pia kulikuwa na makundi matatu ya wanaume.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa walipofika na kukaa kwa muda sehemu hiyo, jirani yake alishuka kwenye gari na alisogea karibu na wanaume waliokuwa wamesimama katika eneo hilo na kuwaeleza kuwa anamtafuta Msangi lakini walimjibu hawamfahamu na baada ya kupewa jibu hilo, alikwenda ndani ya hoteli hiyo.

"Baada ya muda kupita jirani yangu alirejea kwenye gari na alinieleza kwamba ameulizia sehemu ya mapokezi na waliangalia kwenye orodha ya wageni walioingia jina lake halikuwapo.

"Wakati tukitaka kuondoka na gari eneo hilo, tukiwa uelekeo wa kutoka nje ya lango ghafla nilipigiwa simu na mume wangu aliniambia kuwa tusiondoke kwa kuwa yupo kwenye gari jeupe ambalo limepaki hapo. Nilimwambia ateremke kwenye gari aje akajibu amefungwa pingu miguuni.

"Nilishuka kwenye gari langu na kusimama mbele nikiwa natazamana na gari aliloniambia yupo. Muda wa dakika saba kupita, vijana wawili kutoka kundi la tatu walisogea kwenye gari lake na kuniuliza kuwa ni nani aliyeniambia kuwa Msangi yuko eneo hilo.

"Nilimjibu gari ya mume wangu ipo huko na simu yake ina kifaa maalumu cha kukokotoa mawasiliano ya kijografia (GPS), hivyo tulifuatilia na kutambua kuwa yupo na baada ya kuwapa jibu hilo waliniangalia kwa dharau na kurejea kwenye kikundi chao.

"Baada ya dakika chake kwenye mlango wa kuingilia kwenye hoteli hiyo, nilimwona Sabaya akitoka na mkono wa kushoto alikuwa ameshika bahasha ya rangi ya kaki kubwa. mkono wa kulia alikuwa ameshika bastola na alikuwa akiichezea kwa kuirusharusha. Alisogea karibu ya wale vijana na walikuwa wakizungumza mambo ambayo mimi sikufahamu kwa kuwa nilikuwa mbali nao.

Walinzi wa Sabaya waliingia kwenye magari yao wakayawasha wakataka kuondoka ndipo nilikimbia mbele ya geti na kupiga magoti huku nikiwa nimenyoosha mikono, nikimwomba Sabaya kumwachia mume wangu kwa kuwa alikuwa ameemteka nyara na kumweka kwenye gari lake.

"Nikiwa nimepiga magoti nilikuwa namwomba Mheshimiwa Sabaya asimuue mume wangu kwa kuwa yupo kwenye gari lake. Nilimwelekeza kuwa mimi na mtoto wangu ni wagonjwa sana na tunamtegemea yeye.

Nikiwa nalia gari lilisimama mbele yangu, wakashuka vijana wawili wakiwa bunduki mmoja alinipiga nayo mgongoni. Nilipata maumivu makali nikawa nimeanguka chini, aliniambia nisogee njia nilipata maumivu makali kwa kuwa siku si nyingi nilikuwa nimefanyiwa oparesheni ya uzazi.

"Nikawa naendelea kulia na kumwomba amwachie mume wangu wale vijana wawili walinishika bega la kushoto na kulia kuniburuta kunitoa njiani na walinisogeza karibu na gari la Sabaya. Alifungua kioo nilivyomuona nilimwomba asimuue mume wangu hata kama kuna kosa amelifanya basi ampeleke kituo cha polisi. majibu yake aliniambia kuwa nifunge mdomo," alidai.


**MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA**

**STATEMENT OF RECEIPTS AND EXPENDITURE FOR THE YEAR ENDED 31 DEC 2020**

This publication of the Statement of Receipts and Expenditure is made in accordance with regulation 13(a) of the Non Government Organization Act (Amendments), Regulation 2018 which requires Non Government Organizations receiving funds exceeding TZS 20 Million to publish bi annually the funds received and its expenditure.

| DETAILS | ACTUAL - TZS |
|---|---|
| **RECEIPTS** | |
| Opening fund balance | 0 |
| Disbursement from Donors | 1,161,702,466.00 |
| Total Receipts for Donor implemented activities | 1,161,702,466.00 |
| **PROGRAMMES EXPENDITURE** | 689,320,537.00 |
| **OTHER PROGRAMME EXPENDITURE** | |
| Personnel | 522,351,940.00 |
| **TOTAL PROGRAMMES EXENDITURES** | 1,211,672,477.00 |
| **FUND BALANCE** | - 49,970,011.00 |

Fund balance represent an obligation to conduct donor funded activities per contractual commitments made between donor/development partners and the organisation/recipient , where funds have not been transferred and such activities have not yet occurred.

**Executive Director**
**Mtandao Wa Jamii Wa Usimamizi wa Misitu Tanzania(MJUMITA)**
**Plot 323,Msasani Village**
**Mwaikibaki Rd**
**P.O.BOX 21522, Dar es Salaam**
**Tanzania**

216396902

# WHO yataja sababu ya ongezeko vifo corona

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema vifo vya corona vimekuwa vingi awamu hii kwa sababu watu wamekuwa wakifika hospitalini wakiwa wanaumwa kwa kiwango kikubwa huku mapafu yakiwa yameshaharibika.

Mtaalamu anayeshughulikia matatizo ya corona na kujikinga dhidi ya janga hilo, Dk. Nemes Iriya, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati shirika hilo likizungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa huo na chanjo zinazotolewa.

“Kwa sababu ninahusika na matibabu, kuna jambo moja la msingi, taarifa ambazo tunazipata ni kwamba vifo kwenye awamu hii ya ugonjwa ni vingi na moja ya sababu ni wagonjwa wanachelewa kwenda hospitalini. Wanafika hospitalini pale ambapo tayari wameshaumwa sana na tunajua unapofika hospitalini unaumwa sana nafasi ya kukusaidia inakuwa ni ndogo,” alisema.

Dk. Iriya alisema hakuna dawa ambayo inajulikana inatibu corona moja kwa moja bali zilizopo zinasaidia kupunguza madhara ya ugonjwa huo na zinafanya kazi vizuri pale zinapotolewa mapema.

Mgonjwa anapomwenda hospitalini akiwa amechelewa, alisema hata dawa ambazo alitakiwa apewe kusaidia kupunguza madhara ya vifo inakuwa ngumu.

“Mtusaidie watu wawahi hospitalini mapema wanaposikia dalili za corona, ili wasaidiwe

Mapema. Tumeona watu wanakaa nyumbani mpaka mapafu yameshaharibika kabisa ndipo wanakuja hospitalini. Hii inakuwa shida kumsaidia,” alisema.

**WANAONYONYESHA**

Mtaalamu huyo alisema chanjo za corona ni salama kwa wajawazito na wanaonyonyesha.

“Mama aliyejulikana ana corona je, aendelee kunyonyesha? Unyonyeshaji ni salama kwa chanjo hii. Mama anayenyonyesha ana uwezo wa kuendelea kunyonyesha bila tatizo lolote akiwa anafuata kanuni, ambazo amepewa na wahudumu wa afya, kwamba akiwa amevaa barakoa yake vizuri na kuosha mikono vizuri,” alisema.

Kuhusu matumizi ya glovu, alisema WHO haijashauri matumizi yake wakati wa kutoa chanjo, lakini zinaweza kutumika pale mhudumu anapofikiri kuna hatari ya kujiambukiza.

Aidha, kuhusu matumizi ya barakoa, alisema kwa sababu mpaka sasa waliochanjwa ni wachache bado wanaweza kupata corona, hivyo inashauriwa ziendelee kuvaliwa, ili wasibebe kirusi na kukisambaza zaidi.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akizungumza wakati akifungua mkutano wa kwanza wa Chama cha Watawala wa Umma (APAT), jijiji Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali kuboresha mwongozo kudhibiti upotoshaji mitandao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema serikali imeanza kuhuisha mwongozo utakaosimamia uendeshaji wa mitandao ya kijamii, ili kukabilina na upotoshwaji wa taarifa mbalimbali. Msigwa alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na Maofisa Uhusiano na Mawasailiano wa Wizara, Mashirika na Taasisi za Serikali.

Alisema mwongozo huo ulikuwapo, lakini kinachofanyika hivi sasa ni kuuhuisha na mwishoni mwa mwezi huu utatoka na kuanza kutumika kuendesha mitandao hiyo ya kijamii.

Pia, aliwataka Maofisa Habari wa Serikali kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kupambana na watu ambao, wamekuwa wanatumia vibaya mitandao ya kijamii kupotosha umma.

Alisema Maofisa hao wanayo nafasi kubwa ya kuzisemea taasisi za umma katika mambo mbalimbali, ili kuondoa dhana potofu zinazofanywa na watu mbalimbali kwa maslahi binafsi.

“Unakuta jambo linasemwa kwenye mitandao ya kijamii hata zaidi ya wiki Ofisa Habari umekaa kimya tu na jambo likisemwa mara nyingi hata kama la uongo, bila kukanushwa wananchi wanaliamini,” alisema Msigwa.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka kuhakikisha kuwa wanatumia muda wao kutoa taarifa kwa umma zenye ukweli na uhakika, ili kuwasaidia wananchi kupata taarifa zilizopotoshwa.

“Tumieni hii mitandao ya kijamii kuposti kazi za wizara na taarifa zingine muhimu. Unakuta akaunti ya wizara zaidi ya miezi miwili hakuna kitu. Mkifanya hivi wenzenu watazitumia kupotosha na ninyi mpo na hakuna mlichofanya,” alisema.

Pia, alisema katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliana na janga la corona, kwenye mitandao ya kijamii nchini kumekuwa na upotoshaji mkubwa. Alisema hali hiyo ya upotoshaji inawalazimu Maofisa Habari wa Serikali kutumia taaluma zao kutoa elimu na vipindi mbalimbali vya kuelimisha umma juu ya janga la corona wimbi la tatu.

Vilevile alisema kuwa, hivi sasa serikali inalifanyika kazi tatizo la baadhi ya ofisi kuwanyima Maafisa Habari wao mamlaka ya kuzisema pale inapohitajika.

## Maofisa waonywa rushwa ya ngono

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WATAWALA wametakiwa kufanya kazi kwa uadilifu na kuacha tabia ya kiuomba na kupokea rushwa ya ngono na fedha kwa wananchi wanaofika kuomba huduma.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri, aliyasema hayo wakati akitoa hotuba kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, kwenye maadhimisho ya kwanza ya Wataalamu wa Utawala wa Umma Tanzania(APAT) yaliyofanyika jana jijini hapa.

Shekimweri aliwataka watawala hao kusimamia maadili ya sheria za kazi na utumishi wa umma na kukuacha tabia ya kuwarubuni wengine kwa kuwaomba rushwa ya ngono.

“Na hapa niseme kuna baadhi yenu bado wanaendelea na tabia ya kuwarubuni wasichana wanaofika kuomba kufanya mafunzo kwa vitendo. Hilo ni kosa kisheria, unatakiwa kuwajibishwa,” alisema.

Pia, alisema bado kuna baadhi ya watumishi wa umma wanaendelea na tabia ya kuomba rushwa ya ngono wakati wa kutoa huduma kwa wananchi wanaofika kwao. Alisema kuanzishwa kwa umoja huo, kutasaidia kuwakumbusha wataalam na watawala wa umma kuzingatia maadili.

Kadhalika aliwataka kusimamia majukumu kikamilifu pamoja na kusaidia jamii katika tatizo la kuandika barua za maombi ya kazi kwa sababu limekuwa kubwa na kwamba teknolojia imesababisha wengi kushindwa kuandika barua za maombi ya kazi kwa utaratibu na kushindwa kufupisha maelezo ya maombi yao.

Aliwataka kuweka mfumo wa kupima na kujipima kuhusu malengo waliojiwekea kipindi kilichopita baada ya muda na kujiridhisha kabla ya kupanga malengo mapya.

Mwenyekiti wa APAT, Denis Derua, alisema umoja huo ulianzishwa mwaka 2019 na ulipata usajili rasmi mwaka 2021.

Derua alisema mpaka sasa umoja huo una wanachama 158 kutoka Tanzania Bara na visiwani na malengo yake makuu ni kuwaleta pamoja wataalamu wote na watawala wa Umma nchini.

Aliyataja baadhi ya malengo mengine kuwa ni kukuza maslahi, maadili na uwajibikaji katika taaluma ya utawala wa umma na kushirikiana na mashirika na taasisi zingine.

Aliongeza kuwa malengo mengine ni kufanya utafiti, ili kubaini matatizo yanayoikabili taaluma na kutoa ushauri, ili kuleta tija na ufanisi kwa wanachama wote.

Alibainisha kuwa kupitia mkutano huo watapokea mapendekezo na maboresho ya umoja wao, ili kuwahudumia wanachama wake bila kubagua.

# Wafungua shauri kupinga tozo za miamala ya simu

**Na Thobias Mwanakatwe**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimejitosa katika sakata la tozo la miamala ya fedha kwa njia ya simu ambalo linapigiwa kelele na wananchi wengi, kikifungua kesi Mahakama Kuu.

LHRC imefungua shauri hilo namba 11 ya mwaka 2021 kuomba mapitio ya Mahakama Kuu kuhusu 'National Payment System Act Cap 437' pamoja na kanuni zake zilizoweka tozo hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema kesi hiyo ambayo ipo mbele ya Jaji John Mgeta, ilitajwa kwa mara ya kwanza Agosti 5 mwaka huu katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.



Mafundi wakijenga darasa kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji maalum katika Shule ya Msingi Nyambono B, Wilaya ya Musoma, mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA W3ETU**

Alisema LHRC imefungua kesi hiyo kufuatia kupitishwa kwa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Sheria ya Fedha ambayo imeweka tozo katika miamala ya fedha inayofanywa kwa njia ya simu.

Henga alisema kufuatia tozo hizo, kumesababisha mzigo kwa wananchi wa kawaida pamoja na wafanyabiashara wadogo na wakubwa.

"Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilifanya uchambuzi wa hotuba ya bajeti iliyowasilishwa Juni 10, mwaka huu na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuhusu athari ya tozo katika miamala," alisema.

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, itasikiliza tena kesi hiyo kwa mara ya pili Agosti 16, mwaka huu.

Julai 19, mwaka huu, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Nchemba alisema serikali imesikia kilio na maoni ya wananchi kuhusu tozo mpya za miamala ya simu na kuwaomba wawe watulivu wakati jambo hilo linatafutiwa ufumbuzi.

Hata hivyo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, Julai 23 mwaka huu alitoa ufafanuzi kuhusu tozo za miamala kwa kusema kuwa Bunge limepitisha tozo hizo kwa nia njema ya kutekeleza miradi ya maendeleo ili ikifika mwaka 2025 Tanzania iwe imepiga hatua katika maendeleo na kwamba wanaopinga suala hilo, ni vyema wakatoa mawazo mbadala ya nini kifanyike.

Kauli hiyo ya Spika Ndugai ilikuja wakati serikali ikiwa kwenye mchakato wa kupitia na kujadili tozo zinazokatwa kwenye miamala.

# wananchi wasiojiweza kusaidiwa bima ya afya

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 15 kwa ajili ya kuwalipia bima wananchi wasio na uwezo wa kupata huduma hiyo na kazi ya kuwatambua imeshaanza.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Edward Mbanga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa kujadili kuboresha huduma za bima zote nchini.

"Si wananchi wote wana uwezo wa kulipia huduma za afya, hivyo serikali imekusudia kuwatambua kwa kuwatathmini, kuwahoji na kubaini mazingira yao, kisha itachukua dhamana ya kuwalipia. Hadi sasa ni asilimia 14 ya Watanzania ndio waliokata bima ya afya," alisema Mbanga.

Mbaga aliyasema hayo kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, akibainisha kuwa hatua hiyo itawekwa wazi lini itaanza rasmi. Pia aliwataka viongozi wa kampuni zinazotoa bima kujizatiti katika kutoa huduma ikiwamo kutoweka mipaka ya kitita anachohitaji mteja.

"Kitita cha msingi iwe ni haki ya kila anayekihitaji. Ubaguzi wa kumpangia mteja kitita kwamba kwa wewe ununue hiki si sawa. Tanueni huduma zenu zifike vijijini. Itafika wakati usajili wa bima utarahisishwa kama ilivyo kwa usajili wa simu na kitambulisho cha NIDA kitatosha kwa kuwa kina taarifa," alisema.

Alisema muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote uko mbioni kuwasilishwa bungeni mwaka huu na sheria ikipitishwa itakuwa na mambo mengi ambayo yatabainisha huduma hizo za bima kutolewa nchini pote kwa uhakika zaidi.

Mwenyekiti wa Chuo cha Bima na Jamii Afrika, Dk. Baghayo Saqware, alisema wamekusudia kutafiti na kubaini huduma za bima za jamii ambazo hazitolewi ili waanze kuzitoa ikiwa ni hatua ya kuboresha sekta hiyo.

"Katika mkutano huu tunajadiliana mambo kadhaa, humu kuna wataalam wa mausala ya bima pia kuna wanafunzi. Tutapata nafasi ya kuunganisha mawazo mazuri ambayo tunaamini yatasaidia kuboresha huduma zetu hivyo kuwezesha nchi kuwa na maendeleo kupitia sekta yetu," alisema Dk Saqware.

Dk. Heri Marwa, Mkurugenzi wa Pharm Access International alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali hasa upande wa Zanzibar kushauri jinsi ya kusaidia kupunguza gharama za bima kwenye kampuni binafsi ikiwamo kuongezea kwenye gharama za matibabu ya magonjwa makubwa yakiwamo ya figo. Mpangilio wa daladala zinazoegeshwa jirani kama ziendazo Tegeta, Masaki na Mwananyamala uliathirika.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelance Sales Executives

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

Responsibilities

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

Qualifications

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

NOTE: This is a commission Based Position

Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.

616387602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri uchaguzi TFF leo, 'wasaka tonge' waepukwe

**WADAU** wa soka nchini na Watanzania kwa ujumla, leo wanatarajia kupata uongozi mpya wa juu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), katika Uchaguzi Mkuu wa shirikisho hilo utakaofanyika jijini Tanga.

Viongozi watakaochaguliwa katika uchaguzi huo, ni Rais wa TFF pamoja na wajumbe wa sita wa Kamati ya Utendaji huku wajumbe wengine watano wa kamati hiyo ya utendaji wakipatikana kwa kuteuliwa na rais baada ya uchaguzi huo kufanyika.

Kiongozi mwingine wa juu katika shirikisho hilo atakayeingia madarakani leo ni makamu wa rais, ambaye atapatikana kwa kuteuliwa na rais na kisha kupigiwa kura na wajumbe wa mkutano mkuu.

Hata hivyo, Rais wa TFF, Wallace Karia, anayetetea nafasi yake, anachosubiri ni kuidhinishwa tu kuendelea kukalia kiti hicho kutokana na kuwa mgombea pekee aliyekidhi vigezo vyote katika mchakato wa uchaguzi huo ulioanza tangu Juni 8, mwaka huu kabla ya kuhitimishwa baadaye leo.

Hata hivyo, hadi kufikia hatua hii ya kufanyika uchaguzi huo, tunatambua mchakato mzima uligubikwa na mvutano mkubwa na hadi sasa wapo baadhi ya wagombea ambao wamekwenda mahakamani wakipinga namna ulivyoendeshwa kutokana na kutokukubaliana na baadhi ya kanuni ambazo ziliwaengua.

Lakini mahakama haikuona sababu ya msingi ya kuzuia uchaguzi huo kufanyika na kutoa baraka zote, jambo ambalo leo wadau wa soka na Watanzania kwa ujumla watashuhudia viongozi wao watakaokabidhiwa dhamana ya kusimamia mpira wa miguu nchini kwa kipindi kingine cha miaka minne.

Nipashe hatutaki kuingilia uhalali wa waliofikisha kesi mahakamani ama ambao hawakuridhishwa na mchakato mzima wa uchaguzi hadi viongozi hao wanapatikana leo jijini Tanga.

Cha msingi tunachotaka kukiweka wazi kwa wadau wote wa soka na Watanzania kwa ujumla, ni kila mmoja kuona haja ya kushirikiana vema na uongozi utakaopatikana leo katika juhudi za kuhakikisha soka letu linapiga hatua zaidi kutoka hapa lilipo sasa.

Tunatambua hata ambao walienguliwa awali katika mchakato wa uchaguzi huo na wale watakaokosa kura za kutosha leo, wote lengo lao lilikuwa moja tu, kuhakikisha soka la Tanzania linapiga hatua zaidi na kuwa katika viwango vya juu barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Hivyo, kama dhamira yao ilikuwa hiyo, hawatasita kuendelea kuwaunga mkono viongozi watakaochaguliwa leo kwa kutoa michango kwa hali na mali na zaidi mawazo yao kuwa muhimu katika uboreshaji wa soka Tanzania.

Kinyume cha kufanya hivyo, kinatufanya kutambua dhamira na malengo yao makubwa ilikuwa ni kuusaka uongozi huo kwa maslahi yao binafsi na haikuwa kuusaidia mpira wa Tanzania kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa letu.


Tunafahamu wazi, wapo 'wasaka tonge' na si kwa ajili ya kuusaidia mpira wa Tanzania, hivyo Nipashe tunawataka wajumbe wa mkutano mkuu kutowapa kura na hata kama wamefanikiwa kupenya kwa kuchaguliwa ama kuteuliwa katika uchaguzi huo wa leo, basi huu ni wakati sasa wa kuziacha fikra zao 'mfu' na kubadilika mara moja kwa kuwa na mawazo chanya ya kulisaidia soka la Tanzania kwa maslahi mapana ya taifa kwa ujumla.

Aidha, ni wakati sasa wa kuvunja makundi na kambi zote za uchaguzi, na wote kuungana kwa kuwa kitu kimoja katika kulijenga soka la Tanzania, kwa sababu watakaochaguliwa au kuteuliwa leo katika nafasi mbalimbali na wale watakaoshindwa ama waliokosa nafasi hiyo tangu kuanza kwa mchakato huo, wote lengo lao lilikuwa ni kujenga nyumba moja ya soka, hivyo hawana sababu ya kuanza kugombania fito.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge

# Makocha wasiingiliwe usajili



Na Barnabas Maro

**"KOCHA"** ni neno lenye maana zaidi ya moja: (i) Kitendo cha kamba ya nanga kujizonga kwenye mawe chini ya bahari, (2) Kikocha/kikoshi ni kitawi cha matunda yaliyoshikana pamoja kuanzia matatu na kuendelea

Hata hivyo, maana nyingine ya neno "kocha" ni mtu anayetoa mafunzo ya michezo, mkufunzi wa michezo. Pia husemwa mwalimu wa michezo.

Klabu za kandanda duniani kote hutumia mamilioni ya fedha kusajili wachezaji wenye sifa za kucheza kandanda na ambao wataziwezesha timu zao kushinda na kutwaa makombe yanayoshindaniwa. Kwa kawaida usajili wa wachezaji hufanywa na makocha wa timu husika ambao ndiwo wanaojua wachezaji wanaofaa kwa nafasi mbalimbali.

Baada ya hapo huwapa wenye timu majina na idadi ya wachezaji wanaohitajiwa katika nafasi mbalimbali. Hivi ndivyo ilivyo duniani. Kwa hiyo mchezaji anayeshindwa kufanya vizuri, lawama huenda kwa aliyependekeza usajili wa mchezaji/wachezaji walioshindwa kukidhi haja.

Kwa hali yoyote iwayo, makocha ndiwo wanaotakiwa kuchagua wachezaji wanaowataka baada ya kuona uchezaji wao, bidii na nidhamu yao uwanjani. Kwa hakika ndiwo wanaotakiwa kuwatambua wachezaji wanaotakiwa na wasiotakiwa kusajiliwa kwani wana uzoefu huo.

Hivi karibuni Yanga ilimsajili mchezaji wake wa zamani, Haritier Makambo aliyesajiliwa na timu ya Horoya FC ya Guinea ambayo haikumpa nafasi ya kucheza kwa sababu azijuazo kocha wao. Mchezaji huyo aliyekuwa Yanga zamani hakupendekezwa na kocha mpya wa Yanga ila ni mapendekezo ya viongozi wa klabu, na si ya kocha wao, Nasreddine Nabi!.

Swali la kujiuliza ni kwa nini kocha wa Horoya FC ya Guinea, hakumchezesha Makambo kwenye kikosi chake? Aliona hitilafu gani? Kwa sababu hiyo hata kocha Nabi wa Yanga alikuwa na shaka kwa usajili wa Makambo. Je, kama Makambo akishindwa kumridhisha kocha Nabi na kumweka ubaoni tu, waliomleta Makambo watawaambia nini wanachama na mashabiki wa Yanga?

Halahala kwani "Kasi isiyo faida kutenda si ada." Maana yake huwa hapana haja ya kuifanya kazi ambayo haileti faida yoyote ile. Methali hii hutumiwa kuwakanya watu dhidi ya kuingilia kazi na shughuli ambazo hazielekei kuwa faida kwa namna yoyote ile. Watu wengine husema "Kazi isiyokuwa na manufaa kutenda si ada."

Kadhalika, twanasihiwa kuwa: "Majuto ni mjukuu (mwishowe huja kinyume.") Kwa kawaida mtu hajuti kabla ya kulitenda jambo fulani; hujuta baadaye wakati ambapo majuto yake hayatafaa kitu kwa kuwa tayari ameshalifanya jambo lenyewe. Methali hii hutunasihi tuyawazie mambo kabla ya kufanya. Tusifanye mambo ovyo ovyo pasi na kuyawazia ili tusije kujuta baadaye. Unapompa mtu kazi, maana yake umemwamini. Kwa hiyo huna sababu ya kumwingilia katika utendaji wake, ila anapoharibu unamweleza kiungwana.

Hatupaswi kumwingilia mtu kwenye kazi yake. Kwa kuwa ndiye uliyemwamini, mpe nafasi na uhuru wa kufanya kazi yake hata kukupa orodha ya watu anaotaka kufanya nao kazi. Akienda arijojo (hali ya kupotea; hali ya kupoteza mwelekeo) ndipo uingilie ili asiharibu zaidi.

Unapompa mkandarasi kazi usimchagulie wafanyakazi kwani huwachagua wafanyakazi anaoona wanafaa kufanya kazi husika. Kadhalika, makocha wasichaguliwe wachezaji bali waachwe huru kujichagulia wenyewe na kama hawakukamilisha wanachotakiwa kukifanya, basi mikataba yao ndio ivunjwe.

Klabu zetu za kandanda zijiepushe na tabia ya kuingilia kazi za walimu wanaowasajili kwa fedha nyingi kisha kuwatimua baada ya muda mfupi! Kubadili walimu mara kwa mara huwafanya wachezaji kutokuwa na mfumo mzuri unaoeleweka na wachezaji, na hivyo hucheza ovyo bila kuelewana.

Walimu wa kandanda duniani kote huajiriwa kutokana na umaarufu wao kwa timu walizozifundisha na kuangalia tabia zao na wachezaji wanaowafundisha. Pia kuangalia ni kwa nini wanaachana. Je, ni tabia mbaya na kuwadharau wachezaji au waliowaajiri?

Kwa ufupi, viongozi wa timu wanawajibika kwa kila jambo linalohusu maendeleo ya klabu kuanzia klabu, wanachama, wachezaji, walimu na benchi zima la ufundi. Kadhalika, viongozi wafanye kazi zao kwa lengo la mafanikio ya klabu si kujinufaisha wao kwa kile wakiitacho 'kupiga pesa.' Viongozi wenye nia hiyo hawafai katu.

marobarnabas@yahoo.com

HABARI KITAIFA

# Mwalimu matatani tuhuma kumbaka mwanafunzi

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoani Singida linamshikilia Mwalimu wa Shule ya Msingi Misuna, Manispaa ya Singida, Alphonce Festo maarufu kwa jina la Faraja (26), kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita mwenye umri wa miaka 13 (jina limehifadhiwa).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Mutabihirwa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Agosti Mosi, mwaka huu, saa 7:00 usiku katika mtaa wa Misuna, nyumbani kwa mwalimu huyo.

"Mnamo Agosti 1, 2021 majira ya saa 6:40 mchana, Jeshi la Polisi lilipokea taarifa ya kubakwa kwa mtoto mmoja mwenye umri wa miaka 13, ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya msingi Misuna," alisema Mutabihirwa.

Kamanda huyo alisema baada ya taarifa hizo, polisi walifanya uchunguzi na kubaini kuwa mtoto huyo alibakwa na Festo ambaye ni mwalimu wa shule ya msingi Misuna, ambayo anasoma mwanafunzi huyo.

Mutabihirwa alisema uchunguzi wa awali umebaini kwamba chanzo cha tukio hilo ni tamaa ya kimwili na kwamba mbinu aliyotumia mtuhumiwa ni kumhadaa mtoto huyo kwa kumwahidi kuwa atamuoa na kumpeleka nyumbani kwake na kumpatia maisha mazuri na hatimaye kutenda tendo hilo la ubakaji.

"Jeshi la polisi lilifanya msako mkali na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa ambaye bado anashikiliwa wakati taratibu za kumfikisha mahakamani zikiendelea. Tayari jalada la kesi yake limefikishwa kwa mwanasheria na kwamba hali ya afya ya mtoto inaendelea vizuri na anaendelea na masomo," alisema.

Mutahibirwa alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Singida kuachana na vitendo vya ubakaji kwa kuwa ni vya kikatili na husababisha maumivu na magonjwa ya kuambukiza kama vile UKIMWI, mimba za utotoni, athari za kisaikolojia na wakati mwingine vifo.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohammed Moyo, akipatiwa chanjo ya corona juzi katika Kituo cha Afya cha Frelimo, Manispaa ya Iringa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Kortini tuhuma za kusafirisha bangi

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI watatu wa Wilaya ya Rufiji, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kibaha wakikabiliwa na kesi tatu tofauti, ikiwamo ya kukutwa wakisafirisha zaidi ya kilo 80 za dawa ya kulevya aina ya bangi.

Katika kesi ya kwanza, Ali Momboka amesomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Joyce Khoi.

Wakili wa Serikali, Upendo Mono, alidai kuwa Julai 21, mwaka huu katika kijiji cha Tawe, Rufiji mkoani Pwani, mshtakiwa alikutwa akisafirisha kilo za bangi 31.78.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana shtaka lake.

Hakimu Khoi alisema kifungu Namba 29 (b) cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya sura Namba 95 iliyorejewa 2019 kinaelekeza mtu akikamatwa na bangi inayozidi kilogram 20 hatapata dhamana.

Kutokana na sheria hiyo, aliamuru mshtakiwa apelekwe mahabusu mpaka Agosti 19, mwaka huu.

Katika kesi ya pili, Mshamu Tindwa, amesomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Joyce Mushi akidaiwa kukutwa akisafirisha kilo 26.69 za bangi.

Katika kesi ya tatu, Julai 21, mwaka huu aneo la Kikobo mshtakiwa Amada Tindwa alikutwa akisafirisha kilo 30.04.

Washtakiwa wote wamekana mashtaka. Kesi zote zitasikilizwa tena Agosti 19, mwaka huu.

# 'Msiwakaribishe watu wasiovaa barakoa'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuacha tabia ya kuwakaribisha watu kuingia majumbani mwao bila kuvaa barakoa ili kuzilinda familia zao dhidi ya corona.

Amesema kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiwakaribisha wageni mbalimbali wakiwa hawajavaa barakoa wala kunawa mikono hali ambayo inaweza kuchangia kuongezeka kwa maambukizi ya corona kwa familia.

Kiswaga aliyasema hayo jana wakati akizindua chanjo ya corona kiwilaya katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama na kusisitiza kuwa barakoa ni muhimu hata nyumbani hasa wageni wanapokuwa wanawatembelea kwa kuwa haijulikani wanatoka sehemu gani.

Alisema hata wale ambao wanafanya biashara kwa kutumia pikipiki za miguu mitatu (bajaji) wahakikishe abiria wao pia wanavaa barakoa. Pia alisisitiza kuwa wahababari pia wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuelimisha jamii juu ya ugonjwa huo hatari.

Katika hatua nyingine, Kiswaga alitoa onyo kwa watumishi wa idara ya afya wasijihusishe na tabia ya kuuza chanjo hizo kwa wananchi kwa kuwa zinatolewa bure. Alisema hatawavumilia wale ambao wanapishana na maagizo ya serikali kuhusu chanjo hiyo.

Mkoa wa Shinyanga tayari umepokea chanjo 25,000 kwa ajili ya kutoa huduma na kwamba zinaweza kuongezeka kulingana na idadi ya watu ambao watajitokeza kupata huduma hiyo.

Vituo ambavyo vitatumika kutoa chanjo wilayani Kahama ni Halmashauri za Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama na kwa manipaa ni katika vituo vya afya vya Kagongwa, Iyenze, Mwendakulima na Hospitali ya Wilaya.

Katika Halmashauri ya Ushetu ni vituo vya afya vya Nyamilangano, Ushetu na Bulungwa huku katika Halmashauri ya Msalalani katika vituo vya afya vya Lunguya, Isaka na Bugarama.

# Mbunge ataka kurudishwa stendi ya zamani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, ameutaka uongozi wa Manispaa ya Morogoro, kurudisha stendi ya Daladala iliyoko katikati ya mji na kuweka kituo kingine katika eneo la Masika, ili kuepusha ajali, msongamano na usumbufu kwa wananchi.

Abood alisema hayo jana baada kupokea malalamiko ya wananchi na viongozi wa vyama vya usafirishaji wa abiria wakiwamo daladala, bajaji na wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga.

Hali ya manispaa kwenye usafiri, alisema si shwari na imekuwa ikisababisha ajali kwa wanaotembea kwa miguu na usalama wa abiria kutokana na kutokuwapo kwa utaratibu mzuri unaochangiwa na kukosekana kwa vituo rasmi.

Alisema utaratibu wa sasa kati ya vituo vya daladala na bajaji umekuwa ukichangia kuwapo kwa misongano wa magari katikati ya mji kutokana na vituo vilivyowekwa kutokuwa rafiki kwa abiria na vyombo vya usafiri. Alisema hali hiyo inasababisha abiria kusubiri kando ya barabara, ili kupata usafiri.

"Tangu kituo cha daladala cha mjini kugeuzwa kuwa maegesho ya magari binafsi na daladala kutakiwa kutumia kituo kipya cha Mafiga, hali ya msongamano katikati ya mji ni kubwa na inasababisha ajali kila siku, kutokana na abiria kusimama eneo lolote kupanda basi au bajaji" alisema.

Mbunge huyo alitolea mfano eneo la Masika ambako kuna msongamano wa magari na abiria nyakati zote wakati pembezoni mwa barabara kuna eneo la wazi, lakini badala ya kutumika kama kituo kidogo cha daladala, wamepewa watu wanaoendesha michezo ya kubahatisha huku wananchi wakiendelea kuteseka na usafiri.

Ili kumaliza msongamano, alisema manispaa na wadau wa usafirishaji wanapaswa kurudisha kituo kidogo cha zamani cha daladala katikati ya mji na kuwapanga kwa mistari bajaji na daladala wakati hatua zingine zikiendelea.

"Kwa maoni yangu sioni faida ya kuweka maegesho kwa magari binafsi katika stendi ya daladala na kuziacha daladala na bajaji, ambazo zimekosa vituo rasmi na badala yake kuleta msongamano barabarani, hivyo kusababisha ajali kwa abiria wanapopanda au kushuka," alisema Abood.

Ili kukifanya kituo kipya cha daladala cha Mafiga kuwa endelevu, alishauri mabasi ya mikoani yanayopita barabara kuu ya Iringa-Dar es Salaam, yafanyiwe utaratibu wa kuingia na kutoka katika kituo hicho na yale yanayokwenda nje ya manispaa, yahamishiwe eneo hilo kutoka stendi kuu ya Msamvu.

Mwenyekiti wa Waendesha Daladala Manispaa ya Morogoro, Hemed Shabani, alisema viongozi wa usafirishaji ndio wamekuwa chanzo kikubwa cha kuwapo kwa msongamano huo kwa kuwa wanakaa kwenye vikao vya makubaliano kati ya daladala na bajaji, lakini hawasimamii utekelezaji.

Naye Mwenyekiti wa Waendesha Bajaji, Manispaa ya Morogoro, Elmasha Hamisi, alipendekeza daladala zirudi stendi ya zamani na kwa bajaji zinazotoka, Kasanga, Chamwino na SUA zipewe eneo la wazi la soko kuu la Chifu Kingalu.

Pia, alisema bajaji zinazotoka sehemu nyingine ziendelee kubaki eneo la JUWATA na wakipatiwa maoneo hayo watajisimamia na kuondoa msongamano na vurugu.



Meneja Mradi wa kujenga nyumba za makazi wa Kampuni ya Muriya ya nchini Oman, Ghizlane Gouch, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, wakati uzinduzi wa maonyesho ya makazi kwa wakazi Tanzania wanaotaka kununua nyumba nchini humo. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Fedha wa kampuni hiyo, Mohamed Abdallah. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SBL yatangazia neema vijana wapambanaji

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Pilsner Lager, inatarajia kutoa zawadi za zaidi ya Sh. Milioni 50 kwa washindi watano kupitia promosheni mpya ya 'Kapu la Wana'.

Kupitia promosheni hiyo, kila mshindi atajishindia zawadi mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.

Taarifa iliyotolewa jana na SBL, ilisema washindi watakaonufaika na fedha hizo ni kutoka kanda ya Kati, Kusini, Kaskazini, Pwani na Kanda ya Ziwa na kwamba kila mshindi atajipatia vitendea kazi vyenye thamani ya Sh. milioni 10 ambavyo vitamwezesha kuboresha biashara anayofanya na kutimiza ndoto zake.

Kwa mujibu wa Meneja wa Pilsner Lager, Ester Rapahel, shindano hilo ni mahusisi kwa vijana wapambanaji wanaofanya shughuli mbalimbali kama kilimo, uvuvi, saluni, na bodaboda ambao wanatamani kufikia malengo makubwa lakini wanakosa uwezeshwaji hali inayowapunguzia kasi ya kufikia malengo yao na mafanikio kwa wakati.

"Kupitia bia yetu ya Pilsner Lager, tumekuja na kampeni hii ijulikanayo kama 'Kapu la Wana' kwa vijana wapambanaji ili kuwawezesha kufikia malengo yao," alisema Raphael.

"Pilsner ni bia ya vijana wapambanaji, wasiokata tamaa na wenye kiu ya kufikia mafanikio makubwa. Tumeona ni vyema kuwawezesha wateja wetu ambao wana kiu ya kufikia mafanikio kwa kuwapa vitendea kazi ili wazidi kusonga mbele zaidi," aliongeza.

Meneja huyo alisema moja ya vigezo vitakavyotumika kupata washindi ni pamoja na umri usiozidi miaka 35 na mshiriki awe na biashara si zaidi ya miaka miwili pamoja na kuwa mpambanaji mwenye stori ya kuvutia zaidi juu ya namna alivyoanza biashara na wapi anataka kuipeleka biashara hiyo.

"Tunatambua kwamba ujasiriamali na biashara si kitu rahisi. Unahitaji maono, uwekezaji na uvumilivu ili kupiga hatua. Kila mmoja ana namna yake ambayo ameanzisha biashara au kazi anayofanya sasa hivi. Kwa hiyo tunachokifanya ni kuchukua mawazo na stori bora zaidi ambazo zitaamsha ndoto za vijana wengine," alisema.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kupitia kampeni ya kapu la wana, vijana wapambanaji watajishindia zana mbalimbali za kazi zikiwamo mashine za kilimo, mashine za boti, vifaa vya saluni na bodaboda ambazo kwa kiasi kikubwa zitasaidia kuboresha shughuli zao na kuongeza uzalishaji.

"Unachotakiwa kufanya ni kufuatilia matangazo yetu katika vipindi mbalimbali vya redio na utashiriki kwa kupiga namba 0800750203 Bure Kabisa kisha kufuata maelekezo kutoka timu yetu maalumu ya wataalamu wabobezi na baadaye utaeleza biashara yako na namna ambavyo ungetamani bia yetu ya Pilsner ishiriki katika kukuza biashara yako," alifafanua.

"Kushiriki kwa njia ya baa, nunua bia yako ya Pilsner upate namba ya ushiriki. Mawazo bora matano yatapitishwa baada ya timu kujiridhisha na uhalisia wa shughuli ikiwamo kuwatembelea wapambanaji hao katika maeneo yao ya kazi," aliongeza.

# Watuhumiwa wanne wa ujambazi wauawa

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wanne wanaosadikiwa kuwa majambazi, wameuawa wakati wakirushiana risasi na polisi baada ya kukataa kutii amri ya kusimama walipoamuriwa kufanya hivyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna msaidizi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watu waliuawa mpakani mwa Wilaya za Nachingwea na Ruangwa wakiwa kwenye pikipiki mbili usiku eneo la stesheni ya zamani ya reli.

Kitinkwi aliwataja watu hao kuwa ni Maulidi Lwambo na mwingine aliyefahamika kwa jina la Awesu na wengine hawajafahamika majina. Miili ya watu hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi ya Sokoine.

Aidha, Kitinkwi alisema taarifa za kiitelijensia walizozipata ziliwaeleza uwapo wa kundi la majambazi ambalo linafanya uhalifu ndani ya mkoa katika Wilaya za Nachingwea na Liwale na kwamba kundi hilo lilipanga kutekeleza uhalifu wilayani Ruangwa.

Baada ya kupata taarifa hiyo, alisema Jeshi la Polisi liliweka mtego sambamba na doria za magari na pikipiki kwenye maunganisho ya barabara za kutoka Nachingwea na Ruangwa kupitia Nanganga na kuwapata watuhumiwa hao wakiwa wamepakizana katika pikipiki mbili zilizoondolewa namba za usajili.

Kitinkwi alisema watu hao baada ya kufika eneo la stesheni ya zamani, walisimamishwa na askari waliokuwa doria kwa lengo la kuwahoji ili wawajue kama raia wema lakini walikataa na ghafla wakaanza kurusha risasi ndipo askari wakajibu mashambulizi na kuwaua.

Alisema katika majibizano hayo, watu wanne kati ya hao sita walijeruhiwa kwa risasi na kupelekwa Hospitali ya Sokoine huku eneo la tukio wakikutwa wakiwa na bunduki moja aina ya shotgun Na. 09010030 ikiwa na risasi 10 mashuka mawili ya kimasai.

Vitu vingine ni pamoja na simu mbili, begi moja jeusi la kubeba mgongoni, mfuko wa kinamama, panga, vocha 42 za aina mbalimbali za simu, laini za simu, fulana, sweta moja na tiketi ya kusafiria kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam yenye jina la Maulidi Lwambo.



# Wazee wapigiwa chapuo kupata chanjo ya corona

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SERIKALI imewahamasisha wazee kuchangamkia kupata chanjo ya corona kwa kuwa ni kundi ambalo liko kwenye hatari ya kupata maambukizi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, jijini hapa. Alisema wazee ni kundi ambalo liko kwenye hatari ya kupata maambukizi ya corona na jamii iwahamasishe waende kwenye vituo vya kutolea chanjo ili wapate huduma hiyo.

"Tunalisisitiza hili kwasababu wazee ni tunu ya taifa na wanastahili kulindwa ni majanga mbalimbali ikiwamo kuimarisha ulinzi na usalama wa afya zao, uzee na kuzeeka unaambatana na upungufu wa kinga mwilini serikali inatoa wito kwa wazee wote nchini kujitokeza kwa wingi kutumia fursa ya chanjo ya UVIKO-19 (corona)," alisema.

Aliwagiza maofisa ustawi na maofisa maendeleo ya jamii nchini kuhakikisha wanahamasisha wazee kupitia majukwaa mbalimbali yakiwamo mabaraza ya wazee ili wapate elimu namna ya kupata chanjo katika vituo vilivyopangwa.

"Katika kutekeleza jukumu hilo maofisa ustawi, watoa huduma za afya na maofisa maendeleo ya jamii wahakikishe wazee wanapewa kipaumbele katika kupata huduma ya chanjo bila usumbufu wa aina yeyote," alisema.

Aliomba mashirika na asasi za kiraia zinazotoa huduma kwa wazee kuandaa na kuendesha programu mbalimbali za kuhamasisha wazee kwenda kupata chanjo ya corona.

Hata hivyo, alisema hadi sasa kwenye mikoa yote mwitikio upo vizuri na wananchi wengi wanajitokeza.

"Tuna wasiwasi chanjo zitakwisha zilizoletwa kwa awamu ya kwanza kutokana na mwitikio mkubwa. Wengine watalazimika kusubiri awamu nyingine, wananchi wamehamasika na hatujapata changamoto yeyote ya chanjo," alisema.

Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Shilungu Ndaki, alisema wazee wasiojua kusoma na kuandika watatambuliwa mapema na watapatiwa huduma ya chanjo bila bughudha yoyote.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Seleman Jafo (kushoto), akimsikiliza Jordan Ombeni, mwanafunzi wa kidato cha kwanza shule ya St. Carolus ya Manispaa ya Singida, kuhusu utafiti walioufanya wa kilimo cha kutumia maji kidogo kwenye umwagiliaji wa mimea kwenye bustani na kilio, alipotembelea shuleni hapo jana, kujionea utafiti huo utakaosaidia utunzaji mazingira. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Walengwa TASAF wapata soko la zabibu

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WALENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamepata soko la uhakika la zabibu kutoka kwa wanunuzi wa nje na ndani ya nchi.

Kutokana na upatikanaji wa soko hilo, walengwa hao kwa sasa wanauza kilo moja kwa Sh. 1,500 badala ya Sh. 1,000 ilivyokuwa awali. Mtendaji wa Kata ya Handali, iliyoko wilayani Chamwino, Khalfan Mayagila, aliyasema hayo katika ziara ya kutembelea mradi wa shamba lazabibu kwa walengwa hao wilayani hapa.

Mayagila alisema kwa sasa wanapata wanunuzi kutoka Kenya na wengine katika viwanda mbalimbali hapa nchini.

"Msimu huu tunauhakika na zabibu kwa sababu tumepata wanunuzi wengine na ushindani unaonekana kulingana na bei ambazo wananunua," alisema Mayagila.

Alifafanua kuwa mradi huo ulianza mwaka 2016 wakiwa na ekari mbili na nusu.

"Msimu huu tunatarajia kuvuna zabibu nyingi ambazo zitauzwa na fedha zitakazopatikana zitatumika kufanya maendeleo mbalimbali ya walengwa," alisema.

Naye mnufaika wa TASAF, Damalis Mtagwa, aliishukuru TASAF kwa kusaidia kwa kiasi kikubwa kujiinua kiuchumi na kupiga hatua katika kujitegemea.

Alisema katika shamba hilo ambalo limekuwa shamba darasa kwao, kila mlengwa baada ya kujifunza aliamua kutoka na kwenda kuanzisha mashamba yao mengine.

"Kwa kweli TASAF imesaidia wananchi kuinuka kiuchumi kwa sababu kupitia fedha za nguvu kazi ambazo zinatolewa na TASAF zimesaidia sana kuwainua wananchi,"alisema Mtagwa.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Chamwino, Mbegu Yange, alisema wamekuwa wakiwafundisha walengwa namna ya kutumia fedha wanazopewa kujikwamua kiuchumi.

Alisema walengwa wengi wamepiga hatua kubwa na wanafikiria kuendelea kuwa wajasiriamali wakubwa kupitia maarifa waliyopata kwenye mpango huo.

Aliahidi kuwa TASAF itaendelea kutoa elimu kwa walengwa kujitegemea kiuchumi.

# Bila kuvaa barakoa usifanye biashara

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UONGOZI wa Soko la Sabasaba jijini Dodoma umewataka wafanyabiashara kutofanya biashara zao wakiwa wamevaa barakoa na kuweka vitakasa mikono kwenye maeneo yao ili kukabiliana na corona.

Pia watu wote wanaoingia katika soko hilo wametakiwa kuvaa barokoa na kunawa mikono kwa maji tiririka yaliyowekwa kwenye milango ya kuingilia sokoni hapo.

Akizungumza kwa niaba ya uongozi wa soko hilo, Makamu Mwenyekiti Adam Kombo, alisema angalizo hilo ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ambaye ameagiza maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu kujihadhari ya ugonjwa huo.

Kombo alisema pamoja na kuwahimiza wafanyabiashara kuchukua tahadhari pia kwa upande wa watumiaji wengine wa soko hilo, watakaoingia wahakikishe na wao wanavaa barakoa na kunawa mikono.

Alisema kuwa uhamasishaji wa kuvaa barokoa na kunawa maji na sabuni kwa wafanyabiashara na watumiaji wa soko hilo ni endelevu.

"Uongozi wa soko unawashauri wanaoingia kwenye soko hili pamoja na wafanyabiashara wenyewe kuhakikisha wanafuata maelekezo ya wataalamu hao wa afya ili kuepukana na maambukizo ya corona," alisema.

Naye Katibu Msaidizi wa Soko, Victor Challo, alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa hawachukui tahadhari za kujilinda na ugonjwa huo.

Alisema baadhi yao wamekuwa wakiufananisha ugonjwa huo wa corona kama maradhi mengine hivyo hakuna haja ya kuvaa barokoa wala kunawa maji na sabuni.

Ofisa Afya wa Kata ya Viwandani, Fausta Kibiki, alisema kwenye soko hilo kuna maeneo matatu ambayo kuna hatari ya watu kupata maambukizi ikiwa elimu ya ziada haitatolewa kwa upande wao.

Kibiki aliyataja maeneo ambayo yanahitaji kupatiwa elimu ya ziada ya kujihadhari na maambukizi hayo ni pamoja na wanaodakisha mitumba, waendesha bodaboda, wauzaji wa mboga na matunda na eneo la stendi ya daladala wanakopandia na kushusha abiria ndani ya soko hilo.

"Elimu zaidi ya ziada inahitajika kwenye maeneo hayo,kutokana na wingi wa watu na walio wengi hawavai barokoa, na hata hayo maji tiririka pamoja na sabuni hakuna," alisema.

Ofisa huyo aliutaka uongozi huo wa soko kuhakikisha wanashirikiana kwa pamoja katika utoaji wa elimu ili kila mmoja ajilinde na ugonjwa huo.





# Corona yaipaisha teknolojia habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MARADHI ya corona yameshawishi kukua kwa teknolojia ya mawasiliano ya 'zoom' na kusaidia watu mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari kushiriki mikutano na warsha mbalimbali kutumia mtandao huo.

Matumizi ya kasi ya teknolojia hiyo ya mtandao wa 'zoom' yameshika kasi baada ya dunia kukumbwa na janga la corona. Baadhi ya nchi zimesitisha mikutano na warsha ya kuwakutanisha watu ana kwa ana kutoka mataifa mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe, Haji Nassor, mwandishi wa habari kisiwani Pemba, alisema mtandao wa 'zoom' umemsaidia kujifunza mambo mengi kwa kushiriki katika mikutano na warsha mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Haji alisema amekuwa mtumiaji mkubwa wa teknolojia ya mtandao huo baada ya Tanzania kukumbwa na janga la corona ambao umeenea dunia nzima.

"Kabla ya janga hili la corona sikua na matumizi ya 'zoom' na wala siku nafahamu matumizi yake lakini kwa sasa ni mtumiaji mkubwa wa zoom na imenisaidia sana kupata elimu mbalimbali kupitia taaluma yangu ya uwandishi wa habari," alisema.

Alisema licha ya kutohudhuria mafunzo na mikutano mbalimbali kwa njia ya ana kwa ana lakini mtandao huo umemfanya kuwa karibu na waandishi wezake ambao wako nje ya Kisiwa cha Pemba ambao hushiriki katika mtandao wa 'zoom' kwa kujifunza na kupata elimu mbalimbali.

"Nalipongeza sana shirika la kusaidia waandishi wa habari Inter News. Kabla ya corona ilikuwa ikitukutanisha na waandishi wa habari mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kupitia warsha na mafunzo mbalimbali. Licha ya uwapo wa corona haikusita kutupa elimu na kwa sasa huitoa kwa njia ya mawasiliano ya zoom.

Mwajuma Juma, mwandishi mwandamizi wa kisiwani Unguja, alisema mfumo wa mawasiliano kwa njia ya 'zoom' ni mzuri lakini una changamoto zake. Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni gharama ambapo ili kufanikisha kutumia mtandao huo ni lazima uwe na fedha kwa ajili ya intaneti katika simu au komputa ili kutumia mtandao huo.

Mwajuma alisema licha ya gharama ya fedha pia wakati mwingine mawasiliano huwa ya shida ambapo intaneti huwa haikamati, hivyo kushindwa kushiriki katika mkutano au warsha iliyoandaliwa kupitia mtandao huo.

Mkufunzi kutoka Inter News, Ali Haji Mwadini, alisema mafunzo yanayotolewa kwa njia ya mtandao wa 'zoom' yanaepusha msongamano ya watu kukaa pamoja na ni njia mojawapo ya tahadhari ya kujikinga na corona.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud (kulia), akisalimiana na Balozi wa Msumbiji, Agostinho Abaca, aliefika Ofisini kwake Migombani, Mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mfumo kuandaliwa kuendeleza utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, zimekubaliana kuandaa mfumo wa kitaalamu wa kufanya kazi kwa pamoja utakaoleta matokeo chanya ya kuendeleza na kuukuza utalii wa pande hizo mbili.

Mawaziri wa wizara hizo, Dk. Damas Ndumbaro, na Lela Muhamed Mussa, walifikia makubaliano hayo katika mkutano wao wa pamoja uliofanyika mjini Zanzibar.

Walisema wizara hizo zinafanya kazi moja ingawa zinatofautiana katika baadhi ya maeneo, hivyo kuna umuhimu wa kushirikiana kuongeza nguvu za kiutendaji.

Kwa mujibu wa mawaziri hao, mfumo utakaoundwa utakuwa katika sehemu kuu tatu ikiwamo ya maofisa na wataalamu kutoka wizara hizo ikifuatiwa na ya makatibu wakuu na kwa mawaziri husika wa ziara hizo.

Mawaziri hao walikubaliana kuunganisha vivutio vya pande zote mbili katika kuvitangaza ili wageni wanaoingia nchini watambue uzuri wake ili sekta ya utalii Tanzania ipate hadhi kubwa katika ngazi ya kimataifa.

Waziri Lela alisisitiza suala la uaminifu kwa wadau wote wa utalii wa serikali na binafsi katika ngazi zote ili kuupa sifa ya kipekee utalii wa Tanzania.

Alisema kufanya matangazo ya vivutio vya utalii vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika soko la utalii duniani, kunahitaji nguvu ya pamoja kwa vile hiyo ndiyo nyenzo kuu ya kukuza utalii.

Dk. Ndumbaro kwa upande wake alisema vivutio ambavyo havijafanyiwa matangazo ya kutosha vikiwamo vya urithi wa Kiswahili na Mswahili na Urithi wa Uisilamu uliopo kwa karne nyingi katika mikoa mingi ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kiasi kikubwa vitaongeza idadi ya wageni wanaoingia nchini.

Aliitaja mikoa ya Mtwara, Kilwa, Tabora, Lindi, Tanga, Kigoma na visiwa vyote vya Zanzibar kuwa vina urithi huu ambao una soko kubwa kimataifa hasa katika nchi za iliyokuwa Shirikisho la Urusi."Wakati huu ni mwafaka wa kuandaa mazingira mazuri ya kutengeneza faida katika biashara hii ya utalii nchini, hivyo kuna ulazima wa kuondoshwa kwa vikwazo vyote vinavyokwamisha au vinavyoleta sintofahamu ya kusonga mbele kwa sekta hii muhimu ya taifa," alisema.

# Wanahabari wafundwa haki za raia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari visiwani Zanzibar wametakiwa kutambua umuhimu wa haki za kila raia pamoja na kujikita katika kuongeza kasi ya ushawishi wa uwajibikaji kwa taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alipokuwa akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu haki ya raia na uwajibikaji katika ukumbi wa TAMWA, Tunguu Wilaya ya Kati, Unguja.

Alisema waandishi wa habari wana wajibu mkubwa kwenye jamii, hivyo wanapaswa kuwekeza nguvu zao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha haki za kila raia zinakuwapo na kulindwa na kwamba kufanya hivyo ni kutekeleza majukumu ambayo yataisaidia jamii.

Pia aliwataka waandishi wa habari kuhoji pale wanapogundua haki za raia zinakiukwa au kuvunjwa ili haki hiyo ipatikane.

Dk. Mzuri alisema waandishi wa habari wana wajibu wa kuwajengea wanawake uwezo wa kuhoji kuhusu haki zao za msingi ikiwamo usimamizi wa utekelezaji wa miradi inayowalenga moja kwa moja.

Kuhusu suala la uwajibikaji, Mkurugenzi huyo alisema kuna haja kubwa kwa wanaopewa dhamana kuwajibika ipasavyo kwa kuwa kufanya hivyo ni chachu ya mabadiliko.

Pia aliwataka wanahabari kutumia kalamu zao kwa kuhoji na kuifuatilia miradi inayowahusu zaidi wanawake ambayo haifanyi vizuri kwa kuwa ni sehemu ya jamii inayohitaji kuungwa mkono, hivyo kuendelea kukaa kimya hakutawasaidia wanawake ambao ndio sehemu yenye mchango mkubwa kwa jamii.

Akiwasilisha mada ya uwajibikaji na haki za binadamu, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Mzee Mustafa, alisema waandishi wa habari wana dhima kubwa ya kuibadili jamii. Alisema vyombo vya habari vinapaswa kuishawishi jamii kujitambua kuwa ni sehemu ya watu wanaopaswa kushirikishwa katika mipango mbalimbali ya maendeleo.

Alisema iwapo jamii itashirikishwa ni wazi kuwa maendeleo ya haraka yatapatikana sambamba na kuigusa jamii moja kwa moja na yale yote wanayoyahitaji kutambulika kwa urahisi.



MSAMI

Uk.14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI AGOSTI 7, 2021



## PENZI LA KISASI

# Ruby ft Moze Iyobo Aunty Ezekiel ft Kusah

HIVI karibuni mashabiki wa muziki walijumuika kwa wingi katika mitandao ya kijamii, kujadili juu ya penzi jipya linalowahusisha wasanii Hellen Majeshi maarufu kama Ruby na Mose Iyobo.

Kilichofanya mjadala huo kuwa mkali kutokana na penzi hilo ni kama la kisasi, kwani Ruby anaona kusalitiwa na mwigizaji Aunty Ezekiel kwa kumchukua mwanaume wake Kusah.

Kwa upande mwingine Mose Iyobo, moyo wake nado haujakubali baada ya mama wa mtoto wake, Aunty Ezekiel, kumbwaga na kisha kuanzisha uhusiano na Kusah.

Kusah ambaye ni mwanamuziki na Aunty Ezekiel tayari wana mtoto wa kike.

Baadhi ya wachambuzi wanasema penzi hilo ni sawa na kisasi juu ya kisasi, kwani kila 'kapo' inaonekana kufanya hivyo kama kulipiza kisasi kwa mwenzie.

Ikukmbukwe Kusah alikuwa akimtuhumu Ruby kutoka kimapenzi na msanii wa WBC ambaye ni Iyobo, na baada ya kuachana aliamua kuwa karibu na Aunty Ezekiel.

"Kusah ameamua kuwa na Aunty Ezekiel kama kulipa kisasi kwa Iyobo, ambaye wakati wote alikuwa akimtuhumu kutoka na Ruby. Hii sawa na filamu ya kupendeza," amesema Juma Shauri.

Hata hivyo, amesema Iyobo hata kama hakuwa na nia ya kuwa na Ruby, lakini aliamua kuanzisha uhusiano huo kama kuonyesha yeye naye anaweza kuchukua hatua kama hiyo.

"Naamini mapenzi ya aina hii huwa ni vigumu kudumu kwa sababu kila mtu ameanzisha uhusiano kwa nia ya kujionyesha kwamba anaweza kumuumiza mwenzake," amesema Sarah Thomas.

Kuibuka kwa mjadala huo ni baada ya Ruby, kushiriki maoni katika picha ya Mose Iyobo, katika kukumbuka siku ya kuzaliwa kwake.

Aliandika maneno mazito "Happy birthday Baba Cookie, nakupenda sana na unajua".

Andiko hilo liliwashtua watu wengi kiasi ambacho kila mtu alitoa maoni tofauti.

BASI SAWA

## Patrick Kanumba mbona husomeki?



MWIGIZAJI wa filamu za Bongo Muvi, Patrick Kanumba, amemshangaa Gigy Money, kwa kudai wana uhusiano wa kimapenzi, akisema hawezi kufanya kitu kama hicho. Akijibu madai hayo kupitia EATV, msanii huyo amesema, mapenzi kati yake na Gigy Money ni sawa na mbingu na ardhi na kwamba haiwezekani.

"Hapana sio kweli, chanzo chake sijui imetokea wapi mimi nashangaa, sijawahi kuwa kwenye uhusiano naye kabisa hata hao watu wa mitandaoni sijui nao wanatoa wapi nashangaa".

## Msami atafuta la undani



MWANAMUZIKI wa Bongofleva, Msami Baby, amesema msanii mwenzake Barakah The Prince, kwa sasa ameishiwa kiasi ambacho anamsaidia nauli na pesa ya kula.

"Barakah hana pesa ya kunilipa, wakati anaanza kuimba mimi nishaacha kucheza nafundisha na umaarufu ninao, yule ni kijana wangu wakati mwingine hana pesa ya kula namsaidia, namwezesha kwenye bodaboda na namtumia miamala, ili kumsaidia" amesema Msami Baby

Wawili hao wamekuwa wakitupiana maneno mitandaoni kuhusu madai ya kushuka kwa muziki Bongo.



## John Nini arudi na 'Iza Bella'

BAADA ya kimya cha muda mrefu msanii wa kizazi kipya kutoka Denmark, John Nini maarufu kama Neza Music, ametambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Iza Bella'.

Akizungumza na BT, John Nini mwenye asili ya Burundi amesema Julai, mwaka huu alirudi nchini kwake ikiwa ni miaka 25 tangu aondoke na kutengana na ndugu, jamaa na marafiki zake.

"Nilitengeneza wimbo wa kirundi nyumbani, video pia imetengenezwa nchini Burundi. Iza Bela ni ngoma kali unaweza kuisikiliza katika mitandao," amesema

Wimbo huo ameshautupia katika mitandao ya Spotify, iTunes, Google Play, Amazon Music na Tidal na YouTube.

" Tayari ninaweza kukuambia kuwa wimbo huu Iza Bella ni maalumu msimu huu wa kiangazi na majira ya joto na nina amini utapendwa na waafrika wengi kote duniani hasa wale wanaopenda muziki wa Afro Trap Music," amesema. Taarifa zaidi za mwanamuziki huyo unaweza kuzipata kupitia www.johnnini.com.



## Wizz Star kuipaisha Songwe na 'Nichekeche'

MSANII wa Bongo Fleva, Wizz Star, ametamba kuwa wimbo wake mpya, 'Nichekeche', utampaisha na kuleta mapinduzi ya kimuziki katika mkoa wake wa Songwe.

Akizungumza na BT, Wizz Star, amesema wimbo huo ambao atauachia siku ya Jumapili, utaonyesha nguvu yake na kumuonyesha utofauti wake na wengine.

"Nitaendelea kuuwakilisha Mkoa wangu wa Songwe kupitia sanaa, mashabiki wakinipa sapoti nitafika mbali zaidi," amesema

wimbo huo umetayarishwa na Jomba Beatz wa na video imeongozwa na EK chini ya Songwe Empire," amesema Wizz.

## Hawakung'oka hata kwa jembe

**Na Adam Fungamwango**

LEO tuna wanamuziki ambao, walikuwa na roho ngumu. Walikuwa wagumu kuhama kwenye bendi zao licha ya kwamba kulikuwa na majaribio kadhaa ya kutaka kuwachukua, lakini wakang'ang'ana hapo hapo na sababu kubwa ilikuwa ni kutotaka kuwakera na kuwaudhi mashabiki wao, pia wengine walizuia.

**TX MOSHI WILLIAM-MSONDO NGOMA**

Ni mwanamuziki kipenzi kabisa cha Wana Msondo Ngoma, ambaye hawakukubali hata chembe ahame.

Mashabiki wa Msondo walitumia mbinu mbalimbali kuhakikisha haondoki na walifanikiwa hadi Mwenyezi Mungu alipomchukua mwaka 2006, ndipo waliposhindwa kufanya chochote.

Alikaa kwenye bendi ya Msondo kwa miaka 24 bila kuhama, ingawa kulikuwa na majaribio ya hapa na pale yaliyoshindwa.

Katikati ya miaka ya '80 akiwa anakaribia kutambulishwa kwenye onyesho la DDC Mlimani Park ukumbi wa DDC Kariakoo, alinyakuliwa kama kifaranga na mashabiki wake waliovamia hapo na kukodi Taxi, kumpeleka kwenye ukumbi wa DDC Keko, ambako Msondo walikuwa wakifanya onyesho.

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, TOT Plus ilikaribia kumnyakua baada ya kumpa gari na kumvutia maji nyumbani kwake, lakini wadau wa Msondo walizima jaribio kwa kurudisha gharama zote na pia kumnunulia gari lingine.

**NASRI LUBUA-DDC MLIMANI PARK**

Ni mwimbaji wa sauti ya kwanza aliyejiunga na Sikinde kutoka Lola Africa mwaka 1985, kuziba nafasi ya Hassan Rehani Bitchuka aliyekuwa ametumikia Orchestra Safari Sound (OSS) ya mtindo wa Ndekule na baadaye kurudi Msondo.

Nasri ambaye awali alijulikana kwa jina la Francis Lubua aliendelea kukaa kwenye bendi hiyo hadi alipofariki dunia mwanzoni mwa miaka ya 2000.

**ABDUL RIDHWANI -MSONDO NGOMA**

Ni maarufu zaidi kwa jina la Pangamawe. Ni mpiga gitaa la solo kwenye bendi ya Msondo Ngoma. Alijiunga na bendi hiyo akiwa na umri wa chini ya miaka 18 mwaka 1980 akiwa kama mpiga kinanda baada ya kuondoka kwa Waziri Ally kwenda kuanzisha bendi iliyokuja kujulikana zaidi kwa jina la Njenje.

Baadaye akahamia kwenye gitaa la bass kwa muda mfupi, lakini akageuka kuwa mpiga gitaa la solo wa kutegemewa, akirithi mikoba ya Kassim Mponda baada ya kuihama bendi hiyo na kwenda Sikinde. Hadi leo ni miaka 39, bado yuko na bendi hiyo akiendelea na kazi ya muziki.

**HABIB ABBAS-DDC MLIMANI PARK**

Ni mmoja wa waanzilishi wa bendi ya Mlimani Park Orchestra mwaka 1978. Wanamuziki wote waanzilishi, walitoka kwenye bendi hiyo wengine wakarejea na wengine wamefariki dunia, lakini Habib Abbas Jeff Mgalusi yeye bado yupo na bendi hiyo hadi leo. Ni mpiga drums tegemeo wa bendi hiyo aliyejiunga akitokea bendi ya Afro 70 ya Patrick Balisidya. Ameitumikia bendi hiyo kwa miaka 43 sasa.

**SAID MABERA-MSONDO NGOMA**

Ndiye mwanamuziki aliyeweka rekodi ya kukaa kwa muda mrefu kwenye bendi moja nchini mpaka sasa. Alikaa Msondo kwa miaka 46, hadi mwaka 2020 alipofariki dunia.

Alijiunga na bendi hiyo mwaka 1974 akitokea National ya Arusha akiwa na Bitchuka. Awali Mabera alikuwa akipiga trumpet, lakini aligeuka kuwa mpiga solo namba moja wa bendi hiyo, na hiyo ni baada ya kuchukua mikoba ya Abel Bathazal aliyeiacha bendi na kwenda kuunda Dar Intenational mwaka 1977.






## Mfalme Mwovu: Mungu akupi ulemavu, ukakosa mwendo

**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wana msemo wao mmoja hivi. 'Mungu akikupa ulemavu, hakunyimi mwendo.' Wana maana kuwa binadamu anaweza kuwa na matatizo lukuki, lakini baadaye yatatatulika tu. Pia mtu anaweza kuonekana mbaya, lakini sivyo kama anavyoonekana. Upande wa pili ni mtu mwema, ila kuna binadamu walimfanya kuwa hivyo.

Maana nyingine ya msemo huu ni kwamba hakuna mtu mbaya kwa binadamu wote. Hapa leo tutaiangalia filamu ya 'Mfalme Mwovu' ambayo itatueleza kila kitu ambacho nimekizungumza hapa.

Baadhi ya wasanii walicheza filamu hiyo ni mzee Msisiri wa Msisiri aliyecheza kama Mfalme Gotagota, Ally Sheria aliyecheza kama Mzengo, Khadija Rashid aliyecheza kama Anita na Hamdani Ibrahim aliyecheza kama Mgumo.

Kwenye himaya ya ardhi ya Nsangu anatokea kiumbe wa ajabu anayeishi porini. Kwa wananchi wa himaya hiyo kwao ni kiumbe wa ajabu, lakini ni binadamu wa kawaida kwa mwonekano, lakini anaishi porini akiwinda na kula wanyama. Ni kijana tu wa miaka 25, lakini kutokana na kujitenga na himaya hiyo pamoja na mavazi yake, ajabu anaonekana ni kiumbe wa ajabu.

Wasichana waliokuwa wakienda kuteka maji kisimani ndiye waliyemuona na kupeleka taarifa kijijini. Wakati anamkimbia, binti wa mfalme Anita alitaka kuanguka, lakini kijana huyo aitwaye Nzengo alimuokoa. Ikawa kosa. Binti mfalme akatokea tu kumpenda kijana huyo. Wasichana wenzake kijijini wakaanza kumcheka. Mfalme Gotagota akasikia hilo, akakasirika. Lengo ilikuwa ni kwamba, Anita aolewe na askari mkuu Mguno.

Binti mfalme hamtaki Mguno, anamtaka Msengo. Mipango inafanywa kwa mfalme na Mguno kumfanya aonekane mbaya.

Wanaua baadhi ya watu kwenye himaya na kusingiziwa kijana huyo. Anakatwa na kutaka kuuawa na mfalme. Binti anapinga na kudai akiuawa na yeye anajiua. Mfalme anasitisha. Yanafanyika mashindano ya baiskeli kwenye himaya hiyo na atakayeshinda ndiye atamuoa binti mfalme. Mzengo anashinda kwa sababu alifundishwa kwa siri na binti mfalme. Mfalme anasalimu amri anampa mke kijana Mzengo. Kabla ya hapo anataka kujua alipotoka. Mzengo anasema miaka mingi nyuma mama yake alifukuzwa kwenye kijiji hicho, kwa tuhuma za uchawi wakati huo yeye akiwa mdogo. Akaenda kuishi porini hadi mama yake alipofariki na yeye kuishi peke yake hadi umri huo.



# Rihanna sio mwenzetu

MWANAMUZIKI wa marekani mwenye asili ya visiwa vya Barbados, Rihanna, ametajwa kuwa bilionea mpya.

Kulingana na jarida maarufu la Forbes, mwanamuziki huyo anamiliki utajiri wa kiasi cha dola za marekani bilioni 1.7, na kujiunga na mastaa wengine wenye fedha.

Jarida hilo limesema pamoja na muziki, Rihanna amefanikiwa kupitia kampuni yake ya vipodozi inayoitwa Fenty Beauty.

Katika orodha hiyo, Forbes, imemtaja Oprah Winfrey, kushikilia nafasi ya pili.



## Chike Agada arudi kivingine

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya kutoka nchini Nigeria, Chike Agada, amerudi na nyimbo mpya aliyoitambulisha kwa jina la 'Vibrate' akiwa amemshirikisha rapa maarufu mchini humo Psycho YP.

Baada ya ukimya wa muda mrefu bila kutoa ngoma mpya, nyota huyo ambaye zamani alikuwa anajulikana kama Chykay, amerudi kuzindua alama yake ya muziki HM Record, sambamba na kutangaza ujio wa EP yake mpya.


Ukuaji na ujasiri wa Chike Agada ni dhahiri na toleo hili jipya baada ya kuchukua nafasi kwenye eneo la kutunga na kufanya kazi pamoja na wasanii kama Beazy, Timaya, Wizkid, Falz, Davido, Teeto Ceemos, Lola Rae na Wizboyy.

## Joeboy, mapenzi ni mchanganyiko urembo, uchawi

MWANAMUZIKI nguli kutoka Nigeria, Joeboy, amefunguka kuhusu ujio wa albamu yake mpya, akisema itakuwa na jina linaloelezea mapenzi bila kutumia neno upendo.

"Mpango ulikuwa ni kuja na jina linaloelezea mapenzi vizuri, bila kutumia neno upendo, Kwa sababu mapenzi ni mchanganyiko mzuri wa urembo na uchawi," amesema.

Ameongeza kuwa, albamu yake ya kwanza ambayo ilirekodiwa mwaka jana na timu ya watayarishaji pamoja na watangazaji kama Dëra, BeatsbyKO, Killertunes na E Kelly, ilimletea mabadiliko katika maisha yake.





## Sarkodie, aijia juu BET

NYOTA maarufu kutoka nchini Ghana, Sarkodie, amesikitishwa na uongozi wa tuzo za BET, kwa kumtaja mwanamuziki wa Nigeria Burna Boy, kuwa ndiye msanii wa kwanza kuimba Afrobeat na kufanikiwa kujaza ukumbi wa michezo wa Apollo.

Akiongea kwenye Day Break Hitz, Sarkodie amesema Waghana na wengi wamekuwa kwenye BET na walifanya rekodi zingine za kimataifa, lakini kwa sababu haijabainishwa vya kutosha, watu huwa wanasahau na kuifanya Ghana ionekane haifanyi vizuri.


"Tumefanya vizuri sana lakini bado tunaangalia huko nje kwa vile watu wengine wanafanya, sisemi tunapaswa kuwa, lakini angalau Waghana wanapaswa kuthamini wakati huu, tumefanya vitu na bado tunafanya zaidi," rapa huyo amesisitiza.

## Binti wa Dr Dre aishi kifukara

MWANAMUZIKI wa marekani, Dr Dre na binti yake wa kwanza, Latanya Young, wameingia katika majibizano ya maneno baada mtoto huyo kudai amekosa makazi na anaishi ndani ya gari lake.

Latanya alikaririwa hivi karibuni akimlaumu baba yake kwa kumtelekeza na kwamba, anaishi kwa kutegemea msaada wa wasamaria wema.

"Watoto wangu wanatunzwa na rafiki zangu, hawawezi kuishi ndani ya gari kama mimi najaribu kutafuta kazi, ili nijinusuru," amesema.



MAKALA

# Wajasiriamali kuwezeshwa kuimarisha kampuni ndogo na kati kuinua uchumi

Na Sabato Kasika




DUNIA inazidi kuimarika kiuchumi inapitia kwa kasi katika mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo inaongozwa na biashara za wajasiriamali wadogo na wa kati.

Kutokana na mabadiliko hayo shughuli nyingi ulimwenguni zinafanywa na kampuni ndogo na za kati zinazoanzishwa na wajasiriamali.

Kwa mantiki hiyo, wadau wote wa sekta ya masoko ya mitaji wanashauriwa kwenda na mweleke huo ikiwa ni pamoja na kubuni bidhaa na huduma mpya.

Msisitizo unaelekezwa katika kuzijengea uwezo kwa ajili ya matokeo chanya katika maendeleo ya masoko ya mitaji na ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja na hata taifa kwa ujumla.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Dhamana, Nicodemus Mkama, anasema hayo kwenye uzinduzi wa Mpango wa Kuendeleza Kampuni za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEs).

Uzinduzi huo ulifanyika wiki hii, Dar es Salaam, huku akihimiza wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kutumia fursa ya mpango huo kuwekeza kwenye kampuni ndogo na za kati za ujasiriamali ili kuchangia katika uchumi wa nchi.

"Mapinduzi haya yanaongozwa na biashara za wajasiriamali wadogo na wa kati kwani shughuli nyingi ulimwenguni na mataifa kwa sasa zinafanywa na kampuni ndogo na za kati za wajasiriamali," anasema Mkama.

Anasema kuzinduliwa kwa mpango huo, ni matokeo chanya ya ushirikiano wa wadau katika sekta ya masoko na mitaji wenye lengo la kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya sita.

"Serikali ya awamu ya sita inataka kuhakikisha sekta ya fedha inawezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati," anasema.

Anaongeza" Rais amedhamiria kuweka mazingira wezeshi katika kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu, hivyo nasi tunaunga mkono dhamira hiyo,"

### MKAKATI WA UBORESHAJI

Mkama anasema, Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) yana mkakati wa kuendelea kutekeleza na kujenga masoko ya mitaji endelevu, yenye ufanisi na namna ambayo yatatumika kupata fedha.

Anasema, fedha hizo zitatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini na akawahimiza wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujitokeza kutumia fursa hiyo.

"Ninahimiza kujitokeza kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana, itaendelea kujenga mazingira wezeshi na shirikishi kwani ndiyo njia itakayochochea ukuaji wa uchumi," anasema.

Aidha, anasema, kila mdau ana jukumu la kuchukua hatua za kuboresha shughuli zake kwa kutambua jinsi dunia inavyokwenda, hasa wakati huu wa mapinduzi ya nne ya viwanda ikiongozwa na biashara za wajasiriamali.

"Wajasiriamali wadogo na wa kati ni wakati wao huu, kwani shughuli nyingi ulimwenguni zinafanywa na kampuni zao, hivyo ni muhimu kwenda kulingana na jinsi biashara ilivyo duniani," anasisitiza.

Ofisa Mtendaji huyo anasema kwamba mpango wa kuendeleza kampuni za wajasiriamali wadogo na wa kati katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, unatarajia kuwa na matokeo chanya.

"Unatarajia kuwezesha kampuni ndogo na za kati za ujasiriamali kupata fursa ya kuonekana kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa, kuimarisha taswira za kampuni ndogo na za kati za ujasiriamali na kuongeza fursa za uwekezaji," anasema.

Anaongeza kuwa hatua hiyo itasaidia kuwezesha kujenga utamaduni wa uendeshaji wa kampuni kisasa zaidi ikiwa ni pamoja na kuimarisha utawala bora.

"Kwa njia hiyo, zitatumia fursa za masoko ya mitaji, ikiwa ni pamoja na kupata rasilimali fedha kutoka kwa wawekezaji mbalimbali wa ndani na wa kimataifa na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ushauri wa uwekezaji na usimamizi wa rasilimali fedha," anaongeza kusema.

Mkama anaeleza kupitia mpango huo, kampuni hizo zitaweza kupata rasilimali fedha kutoka kwa wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje na kuwezesha kukidhi vigezo vya kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

"Lengo ni kuwezesha serikali na sekta binafsi kugharimia miradi ya maendeleo na kuuza hisa kwa umma, hatifungani za taasisi za serikali," anasema.

### KUKIDHI VIGEZO

Katika uzinduzi huo, Mkama anasema, jumla ya kampuni nane zimekidhi vigezo kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuzitaja kuwa ni Selcom, Raha Beverage, Victoria Finance na Finca Microfinance Bank.

Kampuni nyingine ni African Microfinance Ltd, Techno Image, Reni the Wate Expert na AKM Gilter Ltd.

Anatoa rai kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam na wadau wengine katika masoko ya mitaji, kuhakikisha mpango huo unaleta tija na manufaa kwa kuongeza hamasa kwa kampuni ndogo na za kati kuchangamkia fursa.

"Hatua hiyo inaweza kuzisaidia kutumia fursa zilizopo katika masoko ya mitaji, kuwezesha Watanzania walioko nje ya nchi kushiriki katika uwekezaji kwenye kampuni ndogo na za kati za hapa nyumbani," anasema.

Anasema, anatamani mpango huo pia uongeze hamasa ya uwekezaji kwa kundi la vijana ambao ndio wengi katika jamii na pia kuwezesha wawekezaji zaidi kuwekeza katika kampuni ndogo.

# Hatari ya kufanya kazi ukiwa umekaa

## ■Chanzo cha magonjwa ya moyo, vifo
## ■Tafiti zimebaini muda wa kuketi kazini



Na Christina Mwakangale

NCHI za dunia ya tatu ni kawaida kuona idadi kubwa ya watu wakifanya kazi wakiwa wameketi kwa muda mrefu, licha ya wataalamu wa afya kudokeza ni hatari kiafya.

Wanaoshi kwenye nchi hizo walioajiriwa, kujiajiri au vibarua wanafanya kazi zaidi ya saa nane au tisa kwa siku wakiwa wamekaa chini.

Mfano mzuri ni fundi wa ushonaji wa nguo, ambaye unaishi naye jirani mtaani kwako, unapotoka asubuhi kuelekea kwenye majukumu yako, naye pia huwa amefika katika shughuli yake na kuketi nyuma ya cherehani yake.

Anapokaa hawezi kunyanyuka kama hana kitu kingine cha kufanya, hata unarudi kutoka kazini majira ya jioni, utamkuta ameketi akiendelea na kazi yake.

Keith Diaz, ambaye ni Profesa Msaidizi wa Tiba ya Tabia katika Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Columbia, Marekani anasema baada ya kufanya utafiti kuhusu hatari za kukaa muda mrefu wakati wa kufanya kazi, umebaini kuwa ni moja ya chanzo cha magonjwa.

Anasema kuketi chini muda mrefu kunaongeza hatari ya kupata magonjwa na kufa mapema, na hata kama unafanya mazoezi, haisaidii kukuepusha na maradhi yanayoweza kusababishwa na kukaa chini muda mrefu.

Katika mahojiano na mafunzo kwa wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa (UN), yaliyoongozwa na Daktari Mwandamizi wa Afya ya Umma. Esther Tan, mtaalamu huyo anasema kutokana na uwepo wa janga la corona au ugonjwa wa COVID-19, kufanyia kazi nyumbani kumekuwa jambo la kawaida na kuvuruga mpangilio wote wa maisha.

### MWILI UNAFANYAJE KAZI

Dk. Diaz anasema, ili mwili wote uweze kufanya kazi inahitajika mishipa ya damu kubana na kutanuka kuruhusu damu kupita kwenda kwenye ubongo na inampa mtu hewa safi, uwezo mzuri wa kushiriki katika shughuli zake, lakini kukaa kwenye kiti kuna punguza hali hiyo.

Anasema mtu akiketi chini muda mrefu kwenye kiti, mishipa inashindwa kufanya kazi kwa ufanisi, hivyo kupunguza kiwango cha damu inayozunguka na kuathiri damu inayokwenda kwenye ubongo.

Anafafanua, kawaida namna mtu anavyokaa ni vigumu kwa damu kuzunguka kwa urahisi kutoka miguuni mpaka kwenye moyo na kwenye ubongo, hali ikiendelea uwezekano ni mkubwa wa mtu kupata magonjwa.

### KAZI WIMA SULUHUSHO?

Dr. Diazi anasema kwa sasa baadhi ya ofisi zimekuwa na madawati yanayoruhusu wafanyakazi kusimama wanapofanya kazi.

Hata hivyo anasema mpaka sasa bado hakuna utafiti uliothibitisha iwapo kuna unafuu kwa wale wanaosimama ikilinganishwa na wanaoketi chini muda mrefu.

"Madawati ya kusimama yamekuwa yakipigiwa chepuo na wafanyabiashara wanayoyauza na sio wanasayansi hivyo hivyo wafanyakazi wasijielekeze kwenye kusimama pekee kama suluhisho la kuketi muda mrefu."

Anaeleza kusimama muda mrefu kuna madhara makubwa kwenye mwili wa mwanadamu ndio maana watu wanaofanyakazi inayohitaji kusimama wamekuwa wakikabiliwa na magonjwa mbalimbali.

### KAZI MUDA MREFU

Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema utafiti umebaini kufanya kazi zaidi ya saa 55 kwa wiki kunasababisha ugonjwa wa kuharusi kwa asilimi 35, pia asilimia 17 husababisha hatari ya moyo kushindwa kufanya kazi.

Kitaalamu inashauriwa muda sahihi wa kufanya kazi ni kati ya saa 35 hadi 40 kwa wiki.

Utafiti huo ambao ulifanywa na Shirika la Kazi Duniani (ILO), unaonyesha robo tatu ya watu waliofariki, ilitokana na saa nyingi za kazi, na wengi wao wenye umri wa kati na wazee.

Utafiti wa kwanza kufanywa duniani unaonyesha watu 745,000 walifariki dunia mwaka 2016 kwa sababu za kufanya kazi kwa muda mrefu.

Ripoti hiyo ilibaini kuwa watu wanaoishi Kusini Mashariki mwa Asia na Magharibi mwa eneo la Pasifiki ndio walioathirika zaidi.

Utafiti huo ingawa haukujumuisha takwimu za kipindi cha janga la corona, maofisa wa WHO, wanasema, mabadiliko ya hivi karibuni watu kufanya kazi nyumbani na kupungua kwa kasi ya uchumi, huenda kumeongeza hatari zinazohusishwa na kufanyakazi kwa kipindi kirefu.

"Kuna ushahidi unaonesha kuwa nchi zinapofunga shughuli za kiuchumi, saa za kufanya kazi zinaongezeka kwa karibu asilimia 10," Ofisa wa WHO, Frank Pega anasema.

Ripoti hiyo inasema kufanya kazi kwa muda mrefu kulikadiriwa kuchangia karibu theluhi moja ya magonjwa yote, yenye kuhusishwa na jambo hilo.

### MBINU OFISINI

Ushauri wa Dk. Diaz ni kwamba, badala ya kutumia mitandao ya kisasa ya mawasiliano au simu za mezani baina ya wafanyakazi, vema kunyanyuka na kwenda kumfuata alipo na kuzungumza naye na kurudi katika eneo lako la kazi, itasaidia kufanya misuli kuzunguka na hivyo damu itatembea vizuri na insulini ndani ya mwili itaunguzwa na kuboresha afya.

Pia, ushauri ni kusimama wima kwenye vikao, kuhamasisha kuwa na tabia ya kusimama wima katika mikutano ya majadiliano kazini badala ya kukaa chini muda wote na kuweka baiskeli ya kufanya mazoezi, japo haishauriwi mfanyakazi kufanya mazoezi mpaka kutoka jasho awapo kazini.

Anasema dakika chache za kuendesha baiskeli ambayo inaweza kuwekwa mahali popote au ndani ya chumba cha mkutano inasaidia kwa afya, pia kupanda na kushuka ngazi kwa viwango vichache ni bora kuliko kupanda lifti kila siku.

"Kama unaenda ghorofa ya tano panda ngazi mpaka ghorofa ya ya tatu kisha panda lifti, itasaidia kufanya mapigo ya moyo kwenda kasi na kuunguza insulini katika mwili wako."

### MAZOEZI

WHO, linapendekeza dakika 150 za mazoezi kwa wiki kwa mtu mzima na mtoto dakika 75 kwa wiki.

Pia shirika hilo limesisitiza watu kuangalia namna bora ya kupunguza muda mrefu wa kuketi chini.

Linasema mazoezi yoyote yatakayo sababisha mapigo ya moyo kuongezeka kwa muda fulani ni mazuri kwa afya ya mwanadamu (Cardio exercise), mazoezi hayo yanaweza kuwa kutembea, kuendesha baiskeli, kuogelea, kucheza mpira wa kikapu, soka, au hata kucheza muziki.

Dk. Diaz anasema shughuli yoyote ya kawaida inayoweza kufanyika kwa kuruhusu viungo kuzungusha damu kwa urahisi ni muhimu.

"Ukiwa unafanya kazi unaweza kunyanyuka kwenda kuchukua maji, unaweza kupika huku umesimama, kutoka upande mmoja wa nyumba kwenda mwingine hivi vyote vinamchango mkubwa vikijumlishwa kwenye muda wa kufanya mazoezi kwa wiki."

"Wakati utafiti unaonyesha kufanya aina yoyote ya mazoezi kwa dakika 30 kunapunguza hatari ya kufa kwa asilimia 35, aina yoyote ya kuhakikisha mwili unazunguka hata kama ni kufanya shughuli za kawaida za kila siku za nyumbani kwa muda huo huo kunapunguza hatari ya kufa kwa asilimia 17."

Dk. Diaz anasema jinsi mtu anavyoketi chini muda mrefu wakati akifanya kazi, ndio namna anavyokuwa kwenye hatari kubwa ya kufa haraka ikilinganishwa na yule anayekaa muda mfupi.

"Shughuli zozote zinazofanywa wakati mtu ameketi chini zina hatari kubwa kwa afya, shughuli hizo ni kama kukaa wakati wakufanya kazi, kuendesha gari, kukaa kucheza gemu kwenye kompyuta, au kuangalia runinga muda mrefu."

HABARI KIMATAIFA

# Japan miaka 76 ikikumbuka bomu la atomiki lililoua maelfu

**Tokyo,** JAPAN

JANA Japan imetimiza miaka 76 tangu bomu la kwanza la atomiki kupigwa jijini Hiroshima, huku Meya wa jiji Hilo akiwaasa viongozi wa dunia kuwa na umoja na kushirikiana kama ilivyo kipindi hiki cha corona.

Meya Kazumi Matsui amesema viongozi wawe tayari kuweka chini silaha za kinyuklia kwa kuwa tayari mataifa yalikubaliana kwamba ni angamizo la kiutu

"Silaha za nyuklia ziliendelezwa ili kushindwa vitani, laki kwa pamoja tunaweza kuziondoa. Hakuna jamii ambayo ni endelevu iwapo kutaendelea kuwapo silaha za sumu," alisema Meya huyo jana.

Marekani ilirusha kombora la nyuklia Hadi Hiroshima, Japan, Agosti 6, mwaka 1945, na kujaribu mji huo huku vifo vikiwa 140,000.

Pia, siku tatu baadae ilirusha kombora la pili mjini Nagasaki, na kusababisha vifo vingine 70,000.

Baada ya mashambukizi hayo, Japan, Agosti 15, iliamua kusitisha vita vya Dunia vya Pili.

**AP**



Mtoto akilia mbele ya eneo 'Peace Memorial Park' ambalo ni maalumu kwa walioathiriwa na bomu la atomiki mjini Hiroshima, Magharibi mwa Japan. Jana nchi hiyo ilitimiza miaka 76 tangu bomu la aina hiyo la kwanza duniani kupigwa eneo hilo na kuua watu 140,000 Agosti 6, mwaka 1945. **PICHA: AP**

# Wanajeshi wa Rwanda waongoza mapigano dhidi ya ugaidi Msumbiji

**Mocimboa da Praia,** MSUMBIJI

WANAJESHI 1000 wa Rwanda, wameanza kazi nchini Msumbiji, tangu wapelekwe nchini humo kukabiliana na wapiganaji ambao wamefanya mashambulizi ya uharibifu kaskazini mwa taifa hilo.

Katika kipindi cha wiki mbili, kundi la kwanza la wanajeshi wa kigeni kuwasili nchini humo dhidi ya wapiganaji hao, limeteka eneo muhimu lenye barabara ya makutano;

Lilikuwa likishikiliwa na wapiganaji hao kwa zaidi ya kipindi cha mwaka mmoja uliopita na wamefika katika mji muhimu wa Mocimboa da Praia.

Katika kipindi cha miaka minne wapiganaji hao walichukua udhibiti wa wilaya tano muhimu katika Mkoa wa Cabo Delgado katika eneo la Mashariki la Msumbiji.

Kufikia sasa takriban watu 3,100 wameuawa na wengine 820, 000 kuachwa bila makazi.

Ni miaka minne sasa tangu makundi ya uasi kuchukua udhibiti wa maeneo mengi ya wilaya tano katika Jimbo la Cabo Delgado, Kaskazini Mashariki mwa Msumbiji.

Wakati makundi ya uasi yalipoteka mji wa Palma mwezi Machi, mji wenye utajiri wa gesi ambako kunatengenezwa kiwanda chenye thamani ya dola bilioni 20 kikiwa ni kiwanda cha pili kwa ukubwa barani Afrika, Kampuni ya Ufaransa ya mafuta ililazimika kuacha ujenzi mkubwa katika eneo hilo.

Jeshi la Ulinzi la Msumbiji linafahamika kwa kiasi kikubwa kuwa ni lenye ufisadi lenye mafunzo ya kiwango cha chini na lenye ukosefu wa vifaa na kwamba wasingeweza kukabiliana na mashambulio ya wapiganaji.

Licha ya kupingwa na ndani ya chama chake, Rais Filipe Nyusi alita usaidizi wa nje.

Kuna mapatano mengi mwamko wa uasi ulianzishwa na vijana wasio na ajira wanaopinga kuongezeka kwa umasikini na ukosefu wa usawa, pamoja na ukosefu wa faida zitokanazo na rasilimali, ikiwa ni pamoja na gesi na mawe ya thamani ya rubi.

Mzozo ulianza na shambulio dhidi ya Mocímboa da Praia mwaka 2017 na mzozo huo ukaendelea kuwa mbaya huku vijana wakiteka silaha kutoka kwa wanajeshi na kupata uungaji mkono wa wenyeji.

**BBC**

# Rais Zuma atoka gerezani, alazwa

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amelazwa katika hospitali nje ya gereza kwa ajili ya kufanyiwa uangalizi wa kimatibabu, wamesema maofisa wa gereza.

Wakfu wake umesema kuwa ulikuwa ni uchunguzi wa kawaida wa kimatibabu wa kila mwaka na kwamba hakuna lolote la kutisha.

Kama rais wa zamani wa nchi, Zuma anatibiwa katika hospitali ya jeshi, maofisa walisema.

Rais huyo wa zamani amekuwa akitumikia kifungo cha miezi 15 gerezani tangu alipohukumiwa Julai 7, mwaka huu kwa kutoheshimu agizo la mahakama.

Maofisa wa gereza wanasema kuwa ana haki ya kupata matibabu kama mfungwa mwingine yoyote yule anayefungwa gerezani.

Wizara ya Sheria ilituma taarifa kamili kwenye mtandao wa Twitter.

Wiki ijayo, rais huyo wa zamani amepangiwa kufika mahakamani kwa tuhuma tofauti zinazohusiana na kesi ya ufisadi katika mkataba wa silaha.

Alikana mashitaka ya kuhusika katika mkataba huo wenye thamani ya dola bilioni tano (£3bn).

**BBC**

# Ramaphosa afanya mabadiliko baraza lake la mawaziri

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ameteua Mwenyekiti wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini Enoch Godongwana, kuwa waziri wa fedha akichukua nafasi ya Tito Mboweni baada ya kufanya mabadiliko kwenye baraza lake la mawaziri.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Mboweni alikuwa ameomba kuacha wadhifa huo.

Ramaphosa ambaye alichukua madaraka mwaka 2018 ameapa kuimarisha uchumi, ili kuvutia wawekezaji wakati akikabiliana na ufisadi.

Mabadiliko kwenye baraza la mawaziri yameathiri mawaziri wengine 9 pamoja na naibu waziri 11.

Ramaphosa alisema kuwa amefanya marekebisho hayo, ili kuharakisha uwezo wa serikali wa kutoa chanjo za Covid-19, kufufua uchumi na kuhakikisha udhibiti baada ya ghasia zilizo shuhudiwa hivi karibuni baada ya kufungwa kwa aliyekuwa rais wa zamani Jacob Zuma.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTELEWA NA CHETI



Mimi **BUNANA LUZIGA** nimepotelewa na cheti changu cha kumaliza Kidato cha Nne cha Shule ya Sekondari Mwangaza Mkoa wa Katavi cha mwaka 2007 chenye Namba **S0476-0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa nimeripoti kituo cha Polisi cha Wilaya ya MPANDA nakupewa **KAT/MPA/RB/778341/2020** Kwa mtu yoyote ambae atakiona au kukiokota akipeleke katika kituo cha Polisi kilichokaribu nae.

1163963O2

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ADVENT CONSTRUCTION COMPANY LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CATIC** yenye namba za usajili **T 158 AFY** chasis namba **LNJBLDE154L618838** engine namba **417468,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi; Polisi taarifa **DOD/DOD/RB/384886/2021.**

116392201

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MBUSI NGHABI BUGALI** Wa nyasubi mjini Kahama, Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.586 DQW** aina ya Scania yenye Trailler namba **T. 588 DQW.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi, **KAH/TR/RB/395/2021.**

116397602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TRANSEVENTS COMPANY LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 176 CQY,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **TAN/RB/295139/2021**

116397502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WINNIE ERASTO MWAISEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya HUONIAO yenye namba za usajili MC **772 CAG** chasis namba **LZLIZPq09AHD6152** engine namba **HI157FM0461562,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **TAN/RB/383506/2021**

116397402

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA RUNGWE LILILOKO TUKUYU**

**MAOMBI NA.03/2018**

**LUTH KABETA ..........MDAI**

**DHIDI**

**ANTHONY MWIJALILEGHE..........MDAIWA NA.1**
**MWAKAJWESYA MWIJALILEGHE..........MDAIWA NA.2**
**ENOCK FESTO..........MDAIWA NA.3**
**DAUDI FYEMBE..........MDAIWA NA.4**
**SIMON KIPALA..........MDAIWA NA.5**
**FARAJA LIMBU..........MDAIWA NA 6**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA; ENOCK FESTO,**
**SIMON KIPALA,**
**FARAJA LIMBU.**

Mdai aliyetajwa hapo,amefungua kesi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Rungwe.Mnaarifiwa kufika Baraza la Ardhi na Nyumba tarehe 26/08/2021 saa mbili na nusu asubuhi bila kukosa nyinyi wenyewe au wakili wenu au mtu yeyote mtakayempa maaelezo kamili.

Msipofika kama mlivyoamriwa,shauli hili litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yenu.

AMRI hii imetolewa na mkono wangu na mihuri/lakiri ya baraza hili tarehe 23/08/2021.

R. J. CYRIL
MWENYEKITI WA BARAZA

216396702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

Mimi **PERPETUA YOHANA MWAKAMELA** mwenye S.L.P. 178, Tanga, Mkristo, mtu mzima mwenye akili timamu, naapa na kuthibitisha mbele ya Hakimu/Wakili Mahakam akama ifuatavyo:-

1. Kwamba, Mimi **PERPETUA YOHANA MWAKAMELA** ni mmiliki wa kiwanja Na. 29 Martin shamba area Tanga city.
2. Kwamba, hati ya kiwanja hicho imepotea na nimeitafuta pasipo matumaini ya kuipata tena na kwa uthibitisho nimefika polisi na kupatiwa loss ripoti Na **TAN/TAN/R-B/387345/2021.**
3. Kwamba kwa kiapo hiki naiomba ofisi ya ardhi mipango miji Tanga inipatie hati nyingine kwa jina la **PERPETUA YOHANA MWAKAMELA.**

**UTHIBITISHO**

Mimi **PERPETUA YOHANA MWAKAMELA,** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1 – 3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sharia ya viapo **(The Oaths and Statutory Declaration Act. Cap. 34 R.E. 2021).**

Imethibitishwa hapa Tanga Na
PERPETUA YOHANA MWAKAMELA
Leo tarehe ....................
Mbele ya .................... PERPETUA YOHANA MWAKAMELA
Cheo ....................
Anuani ....................
Sahihi ....................

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

216397202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TELESPHORE NICOLAUS BIDEDERI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUZUKI KEI yenye namba za usajili **T 546 DNM** chasis namba **HN225690178** engine namba **K6A3957520,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/URA/RB/388614/2021**

116395802

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MSTAAFA BUGANYILO ELIAS** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.544 CYL.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/CHU/RB/386252/2021**

116396402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**VINCENT YAHHI QWARAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T163 BFC- TOWNACE NOAH.** Chaisis namba **SR400009382.** Engine namba **3S7142495.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAN/HAN/ RB/387278/2021**

116396602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barupepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 06-08 -2021**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAPILI tarehe 08-08-2021** Kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA** gari hilo lenye namba za usajili **T 366 DLQ/ T 934 AYX**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.8** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.6** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO**

***Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

116397902

## KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA

**Khalifa Twahiri Nyari** Mkazi wa Bomangombe anatangaza kupotelewa na hati ya umiliki wa kiwanja namba **330 Kitalu F Bomangombe** Kwa yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au awasiliane na **KHALIFA TWAHIRI NYARI Kwa namba 0655651999/0766807155 BNG/RB/2799/2018/**

Alphonce R. Lekule
**Kny: KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI, KANDA YA KASKAZINI**

116396802

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Tom alimtazama Tedi kwa jicho la ndani kidogo hadi mwenyewe aliligundua hilo.

"He, mbona umenitazama hivyo?" Alisema huku akitabasamu. Lilikuwa ni tabasamu halisi.

"Tedi?"

"Abee."

"Kwanza pole, sana kwa yote yaliyokukuta. Mimi pamoja na kwamba tumekuja tu hapa ili tuupitishe usiku wa leo, nimeguswa sana na historia ya maisha yako. Kwa hiyo mimi naamua kujitolea kukulipia ada ya kujifunza mambo ya urembo."

Tedi ni kama vile alikuwa kwenye ndoto. Moja ya ndoto chache alizowahi kuota maishani mwaka. Alibaki ameduwaa kama amepigwa ganzi.

"Ni suala la kwenda tu huko na kuuliza ada ni kiasi gani ili nikalipie benki. Halafu napenda niwe mmoja alio ndani ya mafanikio yako, hivyo utakapomaliza mafunzo, mimi nikajitolea kukununulia vifaa vyote vinavyohitajika kwenye saluni."

Ni muda ambao Tedi ni kama alirudiwa na akili ghafla. Akainuka kwenye miguu ya Tom ambayo alikuwa ameilalia. Akamkubatia kwa nguvu kifuani kana kwamba anataka kumkaba. hakutegemea kitu kama kile maishani.

"Hivi ni kweli mpenzi?"

"Siwezi kukudanganya."

"Sasa nifanye nini?"

"Kuhusu nini Tedi?"

"Unataka tena niendelee na kazi hii?"

"Mimi sipendi. Ila endelea kidogo kwa ajili ya kupata pesa za kujikimu, baadaye tutaangalia nini tufanye sasa?"

"Nilikwambia kuwa hata mimi ninaifanya kwa dhiki, lakini si kwa sababu naipenda. Kama umeamua niendelee kwa muda sawa, ila du nashukuru."

Tedi alianza kujihisi kuwa ameanza kuwa mtu mwenye bahati. Maombi yake aliyokuwa akiomba tangu kufariki mama yake na kuishi peke yake akiwa na umri mdogo, anaona Mungu ameanza kumsikia mja wake baada ya miaka mingi.

Mtu ambaye ameshapita na kuwaona wasichana wengi, wa aina mbalimbali. Leo kuamua kumsaidia yeye mambo yake ambayo hayakuwemo kwenye ratiba, wala agenda yoyote. Ni bahati ilioje.




**Kitu kingine ambacho bado kilikuwa kinamuumiza akilini ni kwamba hata kama yote yatafanyika, mkewe Farida akakubali kurudi nyumbani? Kuwa na uhalali wa ndoa ni jambo moja. Lakini ridhaa ya mtu mwenyewe ni jambo lingine. Kwenye maisha ya mahusiano kuna mambo ambayo yanaumiza kichwa sana. Mmoja kama hataki, hata aliyebaki akiwa na uhalali ya ndoa, lakini atabaki tu na cheti chake, lakini mwenzake hayupo nyumbani.**

"Enhe, niambie mpenzi na wewe ni mwenyeji wa hapa Morogoro?" Tedi aliuliza.

Ilikuwa ni zamu wa Tom kushusha pumzi.

"Ni hadithi ndefu." Alisema kwa sauti kama mtu aliyechoka.

Tedi alihisi kuna kitu ambacho huenda si cha kawaida. Huenda mfadhili wake naye ana jambo kubwa. Hata hivyo alisubiri asikie ni kitu gani.

"Mimi naishi Dar es Salaam." Alijibu.

"Nilijua tu. Maana..."

"Nini kimekujulisha mimi si wa Morogoro?"

"Jinsi unavyoongea."

"Naongeaje?" Aliuliza akiwa anampapasa Tedi shavuni.

"Unajua hawa watu wa Morogoro, wakiongea tu kiswahili chao unajua kuwa ni wa huku. Lakini wewe kimenyooka." Alisema na kusababisha wote wawili waangue kicheko na kugongesheana mikono.

"Ni kweli mimi naishi Dar es Salaam."

"Hata mimi nilikuwa nadhani hivyo, kuwa wewe wa mjini kabisa. Si kwa kiswahili hicho." Tedi alizidi kumchekesha Tom.

Maneno ya hawa wote wawili yaliwafanya kila mmoja kusahau shida zake kwa muda.

Tom alijikuta mpaka kama vile anataka kusahau kazi yake ya kumsaka mkewe Farida. Tangu mkewe alipotoroka hadi alipofika Morogoro na kuanza kumsaka huku na kuko, hakuwahi kuwa na amani na furaha kama alivyokuwa sasa.

"Umekuja kikazi?"

Swali hilo ndilo liliomzidua Tom kwenye usingizi mzito. Lililomfanya kuwa ana kazi kubwa ya kujua kisa cha mkewe kumtoroka. Kwa nini yupo Morogoro, tena akitanua na mwanaume mwingine? Kwa nini alikubali kuolewa na wiki moja baadaye kutoroka?

Kitu kingine ambacho bado kilikuwa kinamuumiza akilini ni kwamba hata kama yote yatafanyika, mkewe Farida akakubali kurudi nyumbani? Kuwa na uhalali wa ndoa ni jambo moja. Lakini ridhaa ya mtu mwenyewe ni jambo lingine. Kwenye maisha ya mahusiano kuna mambo ambayo yanaumiza kichwa sana. Mmoja kama hataki, hata aliyebaki akiwa na uhalali ya ndoa, lakini atabaki tu na cheti chake, lakini mwenzake hayupo nyumbani.

Ni kama ambayo hivi sasa imemtokea. Jana alishuhudia kwa macho yake, mkewe akiwa amekumbatiwa na mtu mwingine.

"Nilikwambia kuwa nitakwambia kila kitu. Mimi huku sijaja kikazi."

Wakati Tedi akisubiria Tom aongee kitu alichokitarajia, Tom alibadilisha mada.

"Twende kwanza tukaoge, halafu tuje kulala."

Hakupinga. Alijua tu ataongea baadaye.

Wote walianza kujiandaa kwenda kuoga. Ilionekana wanataka kwenda kuoga pamoja.

"Nenda aoge wewe kwanza." Tom alimwambia Tedi "Siku zote mwanamke lazima apewe heshima yake kwanza."

Alitumia dakika 15 kuoga. Ikawa zamu ya Tom.

"Mbona unakwenda kuoga na mawani?"

"Nikivua sioni vizuri." Tom aliongopa.

Wakati anaoga, ilikuwa ni fursa kwake sasa kurejea kwenye hali yake ya kwaida. Sura ya kawaida. Sura yake halisi. Alivua mawani. Alinyofoa yale madevu aliyoweka. Alijiangalia kwenye kioo na kuiona sura yake halisi.

Kumbuka kuwa alifanya vile ili mkewe asimtambue kule kwenye baa ya Mwenda baada ya kuambiwa huwa anakwenda na mwanaume.

Alijua kuwa akitoka, Tedi atashtuka. Hakuna na jinsi. Ni lazima arejee kwenye hali yake ya kawaida kwa sasa. Labda ikimlazimu baadaye.

Alipomaliza alitoka nje. Mshtuko mkubwa ulimpata Tedi. Alihisi anaota ndoto. Tena ndoto yenyewe mbaya ambayo hajawahi kuota tangu azaliwe. Aliyeingia kuoga, siye aliyetoka.

Alianza kukumbuka hadithi za majini ambao huwa wanajigeuza binadamu. Hata hivyo, hadithi nyingi zilieleza kuwa majini wengi walioijigeuza binadamu ni wanawake. Leo kwa mara ya kwanza anakutana na jini mwaume.

Alitaka kupiga kelele lakini haikutoka. Alijitupa kitandani macho yakiwa yamemtoka, akijua kabisa kuwa kinachofuata ni kuuawa.

Hata kama yule mtu hakuwa jini, lakini alikuwa mtu mbaya na alikuwa na nia mbaya. Alikumbuka pia hekaya wa wanyonya damu. Ambao wanawachukua wanawake, wanawatongoza na kwenda nao kwenye hoteli au nyumba za kulala wageni ni kuwanyonya damu. Sasa ilikuwa ni zamu yake.

Wakati macho yakiwa yamemtoka pima, mikono alinyoosha mbele, ili kujaribu kumzuia mtu aliyetoka bafuni ambaye si yule Tom.

Tom alijua hilo. "Samahani sana Tedi. Mimi ni yule yule mpenzi wako." Tedi mpaka wakati huo alikuwa bado hajalijua jina la mpenzi wake aliyelengeshwa jana na shoga yake. Ila mwenzake alikuwa analifahamu jina lake.

Sauti ilikuwa ni ile ile. Lakini hiyo haikumfanya Tedi kuendelea kuwa na hofu. Mwili wote ulitetemeka na jasho lilimtoka.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**



# GREALISH: NDOTO YANGU IMETIMIA

**MANCHESTER, England**

BAADA ya Manchester City kumsajili kiungo wa England, Jack Grealish kutoka Aston Villa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 100, nyota huyo amesema ametua kwenye timu bora.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, amejiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu England kwa mkataba wa miaka sita na atavaa jezi namba 10 iliyoachwa wazi na Sergio Aguero aliyeondoka.

Ada hiyo imeizima rekodi ya pauni milioni 89 ambayo Manchester United ililipa ili kupata huduma ya Paul Pogba kutoka Juventus mwaka 2016.

"City ni timu bora nchini ikiwa na kocha anayechukuliwa kuwa bora zaidi duniani," alisema Grealish akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni ndoto iliyokuwa kwenye sehemu ya klabu kama hii."

Uhamisho wa Grealish umemfanya kuwa mchezaji wa tisa ghali zaidi katika historia ya soka.

Anaweza kuanza katika kikosi cha Pep Guardiola kwenye mchezo wa leo Jumamosi wa Ngao ya Jamii dhidi ya Leicester City pale kwenye dimba la Wembley.

## MADDISON AWEKEWA NGUMU KUTUA ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA Brendan Rodgers amedai anaamini James Maddison atabaki Leicester City licha ya tetesi kumhusisha na uhamisho wa kwenda Arsenal.



Mchezaji huyo wa zamani wa Norwich ametajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 60 wakati 'Washikabunduki' hao wakionyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo.

Kocha Mikel Arteta si tu kocha anayeiwania saini ya Maddison kipindi hiki cha majira ya joto, kwani klabu yingine ambayo haijatajwa jina nayo inawania saini yake.

Na sasa kocha Rodgers amesema haoni uwezekano wa Maddison kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto.

"Naamini atabakia," alisema Rodgers akiwaambia waandishi wa habari.

"Anajituma sana kwenye mazoezi. Uhamisho wake ni uvumi tu na kama ilivyo kwa miaka mingi. Yeye ni mchezaji muhimu kwenye kikosi chetu.

"Nina matumaini anabaki na sasa na haweza kuondoka kipindi hiki, hilo nina matumaini nalo kwa kiasi kikubwa."

## PIKIPIKI YAUA MTOTO WA BALLACK

**LISBON, Ureno**

MTOTO wa kiume wa mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya Ujerumani na Chelsea, Michael Ballack, Emilio Ballack amefariki dunia baada ya kuanguka kutoka kwenye pikipiki karibu na nyumba ya familia yao nchini Ureno.

Emilio mwenye umri wa miaka 18, alipata ajali hiyo katika Jimbo la Mar karibu na mji wa Troia uliopo Kusini ya mji mkuu wa Ureno, Lisbon.

Polisi wamesema kijana huyo alikuwa akiendesha ukingoni mwa gema wakati pikipiki ilipobiringika nyuma na kumwangukia.

Wafanyakazi wa zimamoto na uokoaji walimtoa kutoka kwenye mabaki ya pikipiki hiyo kujaribu kuokoa uhai wake, lakini juhudi zao zilishindwa na hivyo akapoteza maisha eneo la tukio.

## MADRID WATAJA BEI YA ISCO

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid wametaja bei yao ya kumuuza kiungo wao Isco, baada ya klabu ya AC Milan kuonyesha nia ya kutaka kumvuta katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Madrid wanataka angalau euro milioni 18 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye ameingia miezi 12 ya mwisho kwenye mkataba wake.

Mshahara wa Isco unaweza kuwa sababu kubwa ya kutofanikisha dili hilo endapo AC Milan watashindwa kumlipa mshahara wa sasa anaolipwa katika klabu hiyo wa euro milioni 6.5 kwa mwaka.

Msimu wa 2020/21 ulikuwa mwingine mgumu kwa Isco pale Madrid, akianza michezo nane tu ya LaLiga na akashindwa kufunga msimu wote kwa mara ya kwanza katika taaluma yake nzuri.

Amekuwa akihusishwa na kutakiwa na klabu za Ligi Kuu England huku yeye mwenyewe akibainisha kwamba anataka kupata changamoto mpya.

Machi, mwaka huu, Isco alisema kwamba, kuna uwezekano mkubwa msimu mpya akawa katika klabu mpya, ingawa alisema hajui ni wapi.

## HABARI MICHEZO




# JAMES HAKIELEWEKI MANCHESTER UNITED

**MANCHESTER, England**

WAKATI mashabiki wa Manchester United wakisubiri kuona msimu ujao unakwendaje, baadhi ya wachezaji wana uamuzi wa kufanya, Daniel James ni mmoja wao.

James alijiunga na United mwaka 2019 akiwa miongoni mwa wachezaji watano wa kwanza kusajiliwa (akiwamo Harry Maguire, Aaron Wan-Bissaka, Bruno Fernandes na Odion Ighalo) na Ole Gunnar Solskjaer.

Maisha ndani ya United, yamekuwa ni safari ya kupanda na kushuka kwa James, hii imemfanya winga huyo kukosa namba ya kudumu kwenye kikosi cha timu hiyo.

Man United imekamilisha usajili wa Jadon Sancho, kuongezeka kwa winga huyu, kunaongeza ushindani wa nafasi kwenye kikosi hicho na huenda James akaathirika zaidi kwa kukosa namba kwa muda mrefu.

Ni dhahiri kuwa, James anahitaji kucheza mara kwa mara na kwa sababu hiyo, dirisha hili la usajili ni fursa pekee ya yeye kuondoka United.

Leicester City na Leeds United zinahusishwa na usajili wa winga huyu raia wa Wales.

Leeds United si wageni katika mbio za kuiwania sahihi ya James, walifanya hivyo msimu uliopita bila ya mafanikio.

Manchester United wameweka thamani yake kuwa ni pauni milioni 15 kwa timu yoyote inayomtaka winga huyo.

# NUNO KUMKALISHA KITAKO KANE SPURS

**LONDON, England**

NUNO Espirito Santo amesema hajazungumza na Harry Kane tangu mshambuliaji huyo kutohudhuria mazoezi ya Tottenham Hotspur, lakini anatarajia kuzungumza naye "hivi karibuni".


Kocha mkuu huyo mpya wa Tottenham anaonekana bado hajakutana na Kane, ambaye bado hajarudi mazoezini baada ya kuiongoza England kwenye fainali ya Euro 2020 mwezi uliopita, na alikosa vipindi viwili vya mazoezi ambavyo alitakiwa kuripoti Jumatatu na Jumanne.

Spurs wanatarajiwa kumpiga faini Kane kutokana na kutokuwapo kwake, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anaamini ana makubaliano ya kiungwana na Mwenyekiti Daniel Levy kwamba atauzwa msimu huu wa majira ya joto.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti, Spurs bado haina nia ya kumuuza mchezaji wake huyo kipindi hiki cha majira ya joto.

"Natarajia kuzungumza na Harry hivi karibuni. Bado sijapata nafasi. Lazima kwanza tusuluhishe shida sisi wenyewe, kisha nitazungumza na yeye," alisema Nuno akiwaambia waandishi wa habari baada ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa kirafiki.

"Si kwamba sitaki kutoa maoni, ninachoamini ni kwamba suala hili lote linalohusiana na kila kitu linapaswa kujadiliwa kwa ndani, kati yetu. Wacha tujaribu kuzuia mabishano yoyote ya umma au majadiliano juu yake. Tunapaswa kuzingatia nini ni muhimu, tutatatua hali hiyo, kati yetu.



# ZIYECK AKUNWA NA KIWANGO CHA KANTE

**LONDON, England**

MFUNGAJI wa mabao mawili ya Chelsea, Hakim Ziyech kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Tottenham, ameonekana kufurahia kucheza sambamba na N'golo Kante kutokana na kiwango alichokionyesha kwenye mchezo huo ambao ulichezwa juzi, Uwanja wa Stamford Bridge.

Nyota huyo wa kimataifa wa Morocco, aliifanya Chelsea kuwa mbele kwa mabao mawili aliyopachika dakika ya 16 na 49 kabla ya mabao hayo kusawazishwa na Lucas Moura na Steven Bergwijn.

Akizungumza na Chelsea TV, Ziyech alimwagia sifa Mfaransa huyo kwa kusema, "Kante hushughulikia shida zote nyuma.Kama asipocheza huwa kuna ile hali ya tofauti unaiona uwanjani."

Kuhusu mchezo kwa ujumla,"nafikiri kila kitu tulichokifanya kipindi cha kwanza kilikuwa vizuri. Na bila shaka tunaweza kuhamisha hilo na kucheza vizuri kwa dakika zote 90."

"Ilikuwa jioni nzuri. Kuanzia mwanzo nimefurahia sana. Na nafikiri furaha yangu nimeionyesha uwanjani jinsi nilivyocheza."

"Goli la pili lilikuwa zuri, ni muunganiko mzuri kati yetu na likafanikisha mpira kuingia nyavuni. Goli la kwanza walipoteza mpira, Timo Werner alikimbia vizuri na akatengeneza nafasi kwa ajili yangu. Yalikuwa mabao mawili mazuri."

Ziyech na Kante walicheza pamoja huku pacha nyingine ikiwa kati ya Mateo Kovacic na Kai Havertz ndani ya dakika 45 za kipindi cha kwanza, kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel aliendelea kwenye mchezo huo wa kirafiki kutumia mfumo wake wa 3-4-3.

Mara baada ya mchezo huo wa kirafiki kibarua kilichopo mbele ya Chelsea kwa sasa ni mchezo wa ufunguzi wa msimu mpya wa soka Ulaya, UEFA Super Cup dhidi ya Villarreal, Agosti 11, mwaka huu.

## KWA UFUPI

### KANE BASI TENA CITY

LIONEL Messi anaweza kuathiri uwezekano wowote wa uhamisho ambao Manchester City walikuwa wanaupanga kwa ajili ya mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. ***(Express)***

### AOUAR AIOTA ARSENAL

NYOTA wa Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 23, anasubiri kuhamia katika klabu ya Arsenal kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Sun)***

### LUKAKU HAKIELEWEKI CHELESEA

PENDEKEZO la Romelu Lukaku la kuhamia tena Chelsea huenda likawa linakaribia kukwama kwani mwenyekiti wa klabu ya Inter Milan, Steven Zhang anataka kufikiria kwa muda zaidi kabla ya kuamua iwapo anataka kumuuza mshambuliaji huyo Mbelgiji mwenye umri wa miaka 28. ***(Gazzetta dello Sport)***

### PSG SAHANI MOJA NA MESSI

KLABU ya Paris St-Germain imekuwa ikihusishwa moja kwa moja na Lionel Messi, ambaye ameshindwa kuongeza mkataba kule Bacelona. ***(Le Parisien)***

### TRIPPIER BADO LULU UNITED

MANCHESTER United bado ipo makini na kusaini mkataba na mlinzi wa England, Kieran Trippier, lakini Atletico Madrid wanakataa kupunguza bei yao ya pauni milioni 34 ili kumtoa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Sun)***

### ARSENAL BADO KWA CORREA

ARSENAL wametoa ofa ya dau la takriban dola milioni 17 kwa ajili ya mshambuliaji wa klabu ya Lazio, Joaquin Correa mwenye umri wa miaka 26, ambalo "linatazamwa kuwa halitoshi" na klabu hiyo ya Roma. ***(Corriere dello Sport, via Sport Witness)***

### SOUTHAMPTON KWA ABRAHAM

KLABU ya Southampton wameonyesha nia ya kutaka kumsajili, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23 kutoka klabu ya Chelsea kwa mkopo. ***(Talksport)***

### MESSI AISHITUA MAN CITY

TANGAZO la Barcelona kwamba mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, hatabaki kwenye klabu hiyo "limefungua mlango wa uhamisho wa kushtua" katika klabu ya Manchester City. ***(Manchester Evening News)***

### ARSENAL WAWINDA NYOTA

ARSENAL wanapanga kusaini mkataba na mlinda lango wa England, Aaron Ramsdale na kiungo wa kati wa Norway, Sander Berge kutoka klabu ya Sheffield United, lakini dau la jumla la pauni milioni 50 huenda lisitoshe katika kuwapata vijana hao wawili wenye umri wa miaka 23 kila mmoja. ***(Star)***


### FOFANA AWANIWA LEICESTER

LEICESTER City wamejitokeza katika juhudi za kumuwinda Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 20 raia wa Ufaransa. ***(Sky Sports)***

### MOURINHO AMTAKA ANGUISSA

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, amekuwa akihusishwa na taarifa za kumhamisha kiungo wa kati wa Cameroon kutoka Fulham mwenye umri wa miaka 25, Andre-Frank Zambo Anguissa, ambaye anaweza kuigarimu klabu hiyo ya Serie A takriban pauni milioni 21. ***(Gazzetta dello Sport, via Sport Witness)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, BARCELONA MWISHO WA ENZI

**Alikuwa tayari kuongeza mkataba, lakini vizuizi vya kifedha na kiutawala 'kanuni za Ligi Kuu'...**

**BARCELONA, HISPANIA**

KLABU ya Barcelona imesema mshambuliaji wake nyota, Lionel Messi, hatakuwapo klabuni hapo "kwa sababu ya vizuizi vya kifedha na utawala."

Messi mwenye umri wa miaka 34, amekuwa mchezaji huru tangu Julai Mosi, mwaka huu, wakati mkataba wake ulipomalizika.

Alikubali kusaini mkataba mpya uliokuwa na kipengele cha kupunguza mshahara, wiki mbili baada ya mkataba wa awali kumalizika.

Lakini hali hiyo ilitegemea zaidi Barca kuuza wachezaji ili kumudu mshahara wake.

"Pande zote mbili zimeelezea kusikitika kutokana na matakwa ya mchezaji na klabu kutotimizwa," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Barcelona imesema Messi alikuwa tayari kuongeza muda kusalia klabuni hapo alipodumu kwa miaka 21 kwa kusaini mkataba mpya siku ya Alhamisi, na kulaumu LaLiga kwa kutofanya hivyo.

Tayari alifikia makubaliano ya kukaa na timu hiyo hadi 2026 - lakini LaLiga imesema klabu lazima zipunguze mshahara kabla ya yeye na mchezaji yeyote yule mpya kusajiliwa.

"Licha ya FC Barcelona na Lionel Messi kufikia makubaliano na nia ya wazi ya pande zote mbili kutia saini mkataba mpya leo (juzi), hii haiwezi kutokea kwa sababu ya vizuizi vya kifedha na kiutawala (kanuni za Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga)," klabu hiyo imesema.

"FC Barcelona inatoa shukrani za kipekee kwa mchezaji huyo kwa mchango wake katika kukuza klabu na inamtakia kila la heri katika siku zijazo kwenye maisha yake ya binafsi ya soka," iliongeza taarifa ya Barcelona.

Messi alianza kuichezea klabu ya Barcelona mwaka 2000, amefunga mabao 672 na kushikilia rekodi ya mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo.

# AZAM: HATUPOI HADI FAINALI KAGAME CUP

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam imeserma lengo lao kwenye michuano ya Kombe la Kagame inayoendelea nchini kwa sasa ni kufika hatua ya fainali ili kuendeleza rekodi yao kila wanaposhiriki michuano hiyo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka za Kazi', amesema timu yao ya Azam imekuwa na rekodi ya kufika fainali au kutwaa kombe hilo miaka yote inaposhiriki michuano hiyo ikichezwa popote pale.

Zacharia alisema hayo, mara baada ya Azam juzi kuichapa Le Messager Ngozi ya Burundi bao 1-0 na kutinga hatua ya nusu fainali kwa bao lililowekwa wavuni na mchezaji wa timu hiyo aliyekuwa akiichezea kwa mkopo Namungo FC, Idd Kipanwile.

"Ni historia. Tunataka tuendeleze historia yetu ya kufika fainali, au kuchukua kombe, siku zote michuano hii na sisi tukiwamo. Nia yetu kwanza tuendeleze rekodi yetu na kipaumbele ni kufika fainali ili lengo litimie, halafu baada ya hapo ndiyo tutaangalia hiyo fainali. Kwa sasa siwezi kusema lolote kuhusu fainali," alisema.

Kwenye mechi ya kwanza, Azam iliwatandika Mabingwa Watetezi, KCCA ya Uganda mabao 2-0.

Katika Kundi lake la B, Azam inaongoza kwa pointi zake sita na mabao matatu huku ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutikiswa hadi sasa.

Azam imetwaa kombe hilo mara mbili, mara ya kwanza ikiwa ni mwaka 2015, ilipoifunga Gor Mahia ya Kenya mabao 2-0, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, na kuchukua tena 2018 ilipoifunga Simba 2-1 nchini.

Mwaka 2019, ilipofanyika nchini Rwanda, Azam ilifika hatua ya fainali, ikapoteza kwa bao 1-0 dhidi ya KCCA na haikuchezwa tena michuano hiyo hadi mwaka huu.

UKAGUZI...



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati), akikagua mradi wa Kituo cha Soka Maendeleo cha Mnyanjani kilichoko jijini Tanga. Kulia ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Dar es Salaam (DRFA), Lameck Nyambaya. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Mbeya Kwanza yamfuata Duchu Simba

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya Kwanza umepeleka maombi kwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya kumtaka beki wao, David Kameta 'Duchu' kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa mwaka 2021/22 unaotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu.

Mbeya Kwanza na Geita Gold FC zimepanda daraja na msimu ujao ambao utashirikisha timu 16, zitashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza.

Mwenyekiti wa Mbeya Kwanza, Mohamed Mashango, ameliambia gazeti hili kuwa tayari wamepeleka barua yao kwa Simba na wanatarajia kupata majibu chanya kutoka kwa vigogo hao wa soka nchini.

"Kuhusu usajili kila kitu kinaenda vizuri, katika safu ya ulinzi kocha Matata (Hussein), amempendeza tumpate Duchu, nina imani tutapata majibu mazuri kutoka klabu ya Simba na kupata huduma ya nyota huyo."

"Ligi Kuu itakuwa na ushindani mkubwa, tunatakiwa kufanya usajili mzuri kwa kupata wachezaji wenye uzoefu na uwezo mkubwa wa kupambana na kuleta ushindani mkubwa," alisema Mashango.

Alisema wanapambana kufanya usajili mzuri ili kukijenga kikosi chao kisijekushuka daraja mapema kama timu nyingine zilizoshindwa kukabiliana na ushindani wa ligi hiyo ya juu nchini.

Ihefu FC, Gwambina FC ni miongoni mwa timu zilizopanda Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu uliopita na msimu huu kushuka baada ya kushindwa kuhimili ushindani wa ligi hiyo inayoshika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika kwa sasa.

# SGA yajitosa kuibeba baiskeli

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA, imeahidi kuendelea kuunganisha wakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia michezo kwa kudhamini safari maalumu ya baiskeli ijulikanayo kama 'The Great African Cycling safari' itakayoshirikisha wanamichezo wa nchi tano.

Safari hiyo ilianzia jijini Dar es Salaam mapema wiki hii na kuzinduliwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mbarouk Nasser Mbarouk, ambaye aliongozana na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Dan Kazungu na wadau wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Security, Eric Sambu, alisema ni heshima kubwa kwa kampuni yake kudhamini tukio kubwa kama hilo ambalo litadumu kwa siku 55 na wataendesha kwa umbali wa kilometa 6000 katika nchi hizo tano.

Sambu alisema waendesha baiskeli hao watavuka kuingia Kenya kupitia Tanga halafu wataelekea mjini Mombasa, jijini Nairobi, Kampala, Kigali, Bujumbura, Dodoma na hatimaye kumalizia Arusha ambayo ndiko yalipo makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema Kampuni ya SGA pia itasindikiza msafara huo na kutoa huduma za ulinzi huku ikilenga kuunganisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia kuangalia namna ya kuimarisha biashara kati ya nchi hizi bila vikwazo.

Sambu alisema tukio hilo pia litatumika katika utunzaji wa mazingira na waandaaji wameandaa shughuli za upandaji miti katika maeneo mbalimbali watakayosimama.

**"Tunasafiri zaidi ya Km. 12,000 kila siku kuimarisha biashara katika ukanda huu. Katika kila shilingi inayoguswa Afrika Mashariki angalau senti 80 huwa imesafirishwa na SGA," alisema na kuongeza kuwa SGA imeajiri zaidi ya wafanyakazi 19,000 katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuifanya kuwa kampuni kubwa zaidi ya ulinzi," Sambu aliongeza.**

# Michezo




Jumamosi Agosti 7, 2021
Nipashe

## Messi, Barcelona mwisho wa enzi

HABARI UK. 22

**KWAHERINI...**



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi akiwa na familia yake. Muargentina huyo hatakuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo msimu ujao baada ya klabu yake kushindwa kuingia mkataba mpya kwa sababu ya vizuizi vya kifedha na utawala kutoka LaLiga. **PICHA: MTANDAO**

## Uchaguzi TFF mtifuano mkali nafasi ya ujumbe

**Na Somoe Ng'itu, TANGA**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), linatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu jijini Tanga leo huku ushindani mkali ukionekana zaidi katika nafasi za wagombea wa nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Utendaji.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Kiomoni Kibamba, alisema maandalizi ya mchakato huo yamekamilika na kamati yake itasimamia zoezi hilo kwa kufuata kanuni na taratibu za sheria.

Kibamba alisema anaamini wajumbe wa mkutano mkuu wataitumia vema nafasi yao ya kuchagua viongozi watakaosimamia soka la Tanzania kwa miaka mingine minne kama Katiba ya TFF inavyoelekeza.

"Kila kitu kiko vizuri, tumeshafanya uhakiki wa vifaa vya kazi na naamini Mungu akituamsha salama, mambo yatamalizika kwa wakati na wote kurejea katika majukumu mengine yanayotusubiri," alisema Kibamba.

Alisema nafasi ya Urais inawaniwa na mgombea mmoja ambaye ni Wallace Karia, anayetetea cheo hicho baada ya waliokuwa wapinzani wake kukosa sifa za kugombea kiti hicho cha juu.

Aliwataja wagombea wanaowania Ujumbe wa Kamati ya Utendaji kwa ujumla wake kuwa ni Hoseah Lugano, Athumani Kambi, Lameck Nyambaya, Zakayo Mjema, Khalid Abdallah, Abousufian Silia, James Mhagama, Mohammed Mashango, Hamisi Kitila, Mohammed Aden, Osuri Kosuri, Salum Chama, Salum Kulunge, Vedastus Lufano, Issa Bukuku, Blassy Kiondo na Keneth Pesambili. Kwa upande wa Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, aliliambia gazeti hili kuwa mkutano huo unatarajiwa kufanyika kuanzia saa 3:00 asubuhi na kuhudhuriwa na wajumbe 86.

"Mjumbe mmoja wa TWFA (Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania), ndiye amekosekana, lakini wengine wote tunatarajia watafika hapa Tanga na kutumia haki yao ya kidemokrasia," alisema Kidao.

Alisema mbali na wajumbe hao, pia TFF imewaalika wageni kutoka sehemu mbalimbali kushuhudia uchaguzi huo kutoka ndani na nje ya Tanzania.

# SIMBA MAWINDONI CAF

### ●●● Jembe lingine hadharani leo huku Gomes na nyota wa kimataifa wakirejea tayari kuanza...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha mabingwa wa nchi, Simba kinatarajia kukusanyika Jumapili na kuanza rasmi mazoezi kwa msimu mpya wa mashindano yote ya kimataifa na ya ndani, imeelezwa.

Simba ambayo msimu uliomalizika ilifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, itaiwakilisha tena Tanzania Bara katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF).

Hata hivyo, msimu huu Tanzania itaingiza timu nne katika michuano ya CAF ambapo Ligi ya Mabingwa itawakilishwa na Simba na Yanga, huku Kombe la Shirikisho Afrika, jukumu hili likiwa kwa Azam FC na Biashara United ya Mara.

Simba ambayo ilitoa mapumziko mafupi kwa wachezaji wake baada tu ya kutwaa Kombe la FA, Julai 25, mwaka huu, imelazimika kurejea kambini mapema kutokana na michuano hiyo ya CAF kutangazwa kuanza Septemba 10, ikiwa ni siku 19 kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza.

Kaimu Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ezekiel Kamwaga, amesema baadhi ya wachezaji kutoka nje ya nchi wameshaanza kuwasili, huku wachezaji wa Kitanzania wakiwa tayari wapo, Dar es Salaam.

"Tunaanza rasmi mazoezi Jumapili na nadhani baada ya hapo tutaingia kambini moja kwa moja kujiandaa na msimu mpya wa ligi na mechi za kimataifa kwa sababu muda ni mchache," alisema.

Kamwaga alisema kuwa Kocha Mkuu, Didier Gomes, alitarajiwa kuwasili wakati wowote ule kuanzia leo kuungana na wachezaji wake.

Kuhusu wachezaji wapya, Kaimu Ofisa Habari huyo alisema tayari Kamati ya Usajili wa Klabu ya Simba kwa asilimia kubwa imeshamaliza kazi yake, na kilichobaki ni kuanza tu kuwatangaza ambao wamesajiliwa na klabu hiyo.

"Wanachama na mashabiki wa Simba wakae tayari tu, tutadondosha kitu, kabla ya Jumapili tayari tutakuwa tumemtangaza mchezaji mwingine," alisema Kamwaga.

Simba ambao ni Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara misimu minne mfululizo na Mabingwa wa FA mara mbili mfululizo, mbali na Ligi ya Mabingwa pia wanaanza mazoezi kujiandaa kutetea makombe yao hayo, pamoja na mchezo wa kufungua msimu mpya kuwania Ngao ya Jamii Septemba 25, mwaka huu dhidi ya Yanga.

Simba huenda ikacheza mechi za awali za Ligi ya Mabingwa Septemba 11, mwaka huu, ikiwa na malengo ya kuvuka hatua ya robo fainali ambayo iliishia msimu huu na kuiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 12 zilizopata nafasi ya kuingiza timu nne kila moja katika michuano hiyo ya CAF.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >